




**Waziri** Mkuu: Wenye ulemavu watashirikishwa mchakato wa Katiba mpya

UKURASA 3


Spotika
WACHEZAJI WA5 WENYE MAONO BORA ZAIDI DUNIANI

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Agosti 7, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581395

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


# Moto lori la mafuta watikisa Dar saa 2

• **Dereva**, utingo waokolewa, bodaboda, maduka yaungua, barabara yafungwa... *Endelea ukurasa 2*







Lori la mafuta lililoteketea kwa moto Kimara Kibo, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia akoshwa kibegi Simba

UKURASA 2



# Hatima kesi ya mkataba DP World leo

UKURASA 4

MICHEZO GAMONDI ATAKA MABAO YA SIMBA UK.24 KATUNI UK.6



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Geofrey Mkamilo (kushoto), akitoa maelezo ya miche bora ya parachichi kwa baadhi ya watafiti waliotembelea kitalu hicho katika maonesho ya Nanenane jijini Mbeya jana. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Moto lori la mafuta watikisa Dar

**Na Jenifer Gilla**

LORI lililokuwa limebeba mafuta ya dizeli limepinduka na kuwaka moto katika eneo la Kimara Kibo, wilayani Ubungo, Dar es Salaam na kusababisha maduka na pikipiki zilizokuwa jirani na eneo hilo kuteketea na kuacha vilio na simanzi kwa wamiliki wake.

Ni tukio lililotokea jana saa tano asubuhi wakati gari hilo likielekea Bukoba mkoani Kagera, likapata ajali katika eneo hilo na kusababisha madhara yaliyojumuisha kufungwa kwa barabara kuu ya Morogoro kwa takriban saa mbili.

Akiwa eneo la tukio, Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Kinondoni, Elisha Mugisha, alisema gari hilo lilikuwa linatoka Bandari ya Dar es Salaam, likipeleka mafuta hayo Bukoba, mkoani Kagera.

Alisema dereva na utingo wake walipata majeraha madogo ambayo hayahusiani na moto wakati wanaruka kutoka katika gari hilo na walipatiwa huduma ya kwanza mara moja.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Blasidi Nguwi, alisema aliona lori hilo likigonga nguzo iliyokuwa pembeni mwa barabara kisha kupinduka katika mtaro.

"Nilikuwa hapa ndani nikasikia lori limegonga pale Kibo na kuanguka, kichwa ndicho kilianza kuanguka halafu lile tangi lililokuwa na mafuta likafuata, lilipoanguka ndipo moto ukaanza kuwaka na kusambaa kwa kasi, kadri muda ulivyosogea hadi likaisha kabisa," alisema.

Blasidi alidai moto huo ulifika katika duka lake na kuunguza bidhaa zote pamoja na pikipiki mbili zilizokuwa zimeegeshwa karibu na eneo la tukio. Alikuwa hajafahamu hasara halisi aliyopata.

Dereva wa pikipiki iliyoungua, Daru Omari, alisema baada ya ajali hiyo, ulilipuka moto mkali. Alikimbia na kufanikiwa kujiokoa na kuacha pikipiki eneo hilo ambayo ilifikiwa na moto. Ikateketea.

Alilitaja ni tukio linalomrudisha kwenye maisha magumu kwa kuwa alitegemea pikipiki kupata riziki iliyomwezesha kutimiza mahitaji ya familia yake.

James Aphonce, shuhuda mwingine wa tukio hilo, alidai moto huo haukusababisha madhara makubwa kutokana na mafuta kumwagika mtaroni hivyo moto huo kutosambaa katika makazi ya watu.

"Ulivyoanza kuwaka sisi tukajua ni moto tu wa kawaida, lakini kadri ulivyokuwa unasogea ndivyo ulivyozidi kuwa mkubwa na ukawa ukapaishwa na upepo na kudondokea katika hivi vibanda vilivyopo karibu.

"Tulipoona ile hali ndipo tukawapigia polisi walioko karibu, wakaja tukashiriki kuzima vibanda hadi gari la Zimamoto lilivyofika," alisema.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema walifika eneo la tukio haraka na kudhibiti moto usilete madhara makubwa ikiwamo kuzuia vyombo vya usafiri na watu kupita hadi ulipozimwa.

Pia alisema walifanikiwa kudhibiti wezi waliotaka kutumia tatizo hilo kama fursa ya kuwaibia wafanyabiashara wenye maduka na bidhaa karibu na eneo hilo.

Kwa mujibu wa Kamanda Muliro, mpaka wanadhibiti moto huo saa saba mchana, hakukuwa na taarifa ya mtu yeyote kudhurika. Wanaendelea kufanya uchunguzi wa kina kujua chanzo cha ajali hiyo na kama kuna madhara yoyote yaliyotokea.

"Tumechukua tahadhari zote za kiusalama, tunataka adha ya barabara kutopitika isiwe kubwa, ndiyo maana maofisa wa usalama barabarani wapo hapa wakati tunamalizia jambo hili.

Maeneo mengine lazima yaanze kufanya kazi," alisema Kamanda Muliro akiwa eneo la tukio.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema ulinzi na usalama katika eneo hilo umeimarishwa na hakuna madhara yoyote makubwa yaliyojitokeza.

Alilipongeza Jeshi la Polisi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kufika eneo la tukio mapema. Kulisaidia kudhibiti moto huo kabla haujasababisha madhara makubwa kwa watu wa eneo hilo na mali zao.

Chalamila aliwataka wananchi kuchukua tahadhari linapotokea janga kwa kukaa mbali kwa kuwa moto unaweza kusababisha madhara makubwa kwa mali na binadamu.

"Watu mara nyingi wanapenda kupiga picha mpaka kulisogelea tangi, jambo ambalo lingeweza kuwa kubwa kama lile tukio la Morogoro.

"Kwahiyo, tunachoweza kumshukuru Mungu ni mpaka sasa hatujapata madhara makubwa yaliyosababishwa na ajali hii," alisema.

# Samia akoshwa na kibegi cha Simba, aitaja Yanga

**Na Adam Fungamwango**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameeleza kufurahishwa na ubunifu wa kibegi uliofanywa na klabu ya Simba kukipandisha juu ya Mlima Kilimanjaro.

Ameitaja hatua hiyo imeunga mkono juhudi zake za kukuza utalii aliouanzisha kupitia filamu yake ya Tanzania The Royal Tour.

Akizungumza jana katika Tamasha la 15 la klabu hiyo lililopewa jina la Siku ya Simba, Rais Samia alisema ulikuwa ni ubunifu wa aina yake ambao unapaswa kungwa mkono.

"Michezo huwaleta watu pamoja na huleta amani, maendeleo na mshikamano, kwa sababu kuelekea kwenye kilele cha Simba Day wanachama na mashabiki wa Simba walifanya mambo ya kijamii ikiwamo kwenda kuchangia damu salama kwa ajili ya wahitaji, kujenga wodi ya watoto.

"Simba pia wameitangaza nchi kwenye sekta ya utalii kwa kupeleka kibegi, kimeitangaza sana Tanzania na ulikuwa ni ubunifu wa hali ya juu ambao umeunga mkono juhudi zangu kwenye Royal Tour," alipongeza Rais Samia.

Mkuu wa Nchi pia aliitaka sekta binafsi kuunga mkono jitihada za serikali kwa kuwekeza katika michezo ili kukuza jina la nchi, huku akiahidi kuwa serikali imeandaa mazingira mazuri ili michezo ichezwe kwa amani.

Pia aliahidi klabu zitakazoshiri michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika; Simba na Yanga na Kombe la Shirikisho; Azam FC na Singida Fountain Gate ataendelea kutoa zawadi kwa kila bao moja watakalofunga katika mashindano hayo kama ilivyokuwa msimu uliopita.

"Ahadi ipo palepale, nendeni mkalete ushindi ileteeni sifa Tanzania, ahadi ipo palepale," Rais Samia alisisitiza.

Alipongeza Simba na Yanga kwa kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa msimu uliopita.

"Nimetembezwa sehemu mahsusi ya historia ya klabu yenu. Kwa kweli mnastahili kusifiwa kwa mafanikio mkubwa kimataifa. Mwaka 1974 mlifika nusu fainali ya klabu bingwa barani Afrika na 1993 timu yenu ikacheza fainali ya Kombe la CAF.

"Msimu uliomalizika mkacheza robo fainali Ligi ya Mabingwa, lakini ninawapongeza watani wenu Yanga kwa kufika fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, bila kuisahau timu ya taifa ya wanawake chini ya miaka 18 ikitwaa Kombe la CECAFA kwa kuifunga Uganda bao 1-0," alisema huku akishangiliwa na wapenzi wa michezo waliojitokeza kwa wingi katika uwanja huo.

Rais pia alisema serikali inaendelea kuboresha sekta ya michezo nchi kupitia mikakati mbalimbali, ukiwamo ujenzi wa viwanja vipya.

Alisema tayari yameshaanza maandalizi ya kujenga viwanja vipya Arusha na Dodoma vitakavyochukua watazamaji 30,000 kila kiwanja, ikiwa na maandalizi ya kuwa mwenyeji wa Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) mwaka 2027. Tanzania imeomba kuandaa fainali hizo ikishirikiana na majirani Kenya na Uganda.

"Tayari tumeshapeleka maombi, tunasubiri majibu," alisema Rais na kueleza kuwa timu ya wataalamu iliyotumwa na CAF kuja nchini kukagua miundombinu ya viwanja na hospitali imevutiwa nayo.

Rais aliingia uwanjani na kupokewa na viongozi wa soka nchini pamoja na klabu ya Simba na moja kwa moja kupelekwa eneo maalum ambalo viongozi wa timu hiyo walikuwa wameliandaa kwa ajili ya kumpatia historia ya klabu hiyo.

Baada ya hapo aliingia uwanjani na kupungia maelfu ya mashabiki waliofurika, kabla ya kwenda kusalimiana na wachezaji wote wa klabu ya Simba.

Alipomaliza alisalimiana pia na wachezaji wa Power Dynamos na tukio lililofuata, alipiga picha na wachezaji wa pande zote mbili.

Alianza kupiga na wachezaji wa Simba, baadaye wa Power Dynamos, akapiga na viongozi wao kabla ya kupiga na viongozi wa Simba.

Rais Samia alikwenda kupungia mashabiki waliokuwa wamejazana majukwaani na tukio lililofuata ilikuwa ni kukabidhiwa jezi na viongozi wa klabu hiyo pamoja na tuzo maalum.

Katika tamasha hilo, Rais pia alikaribishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, ambao ni miongoni mwa wadhamini wa tamasha.

## HABARI KITAIFA

# PM: Wenye ulemavu kushirikishwa mchakato Katiba mpya

**Na Enock Charles**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itasimamia kikamilifu kuhakikisha kundi la watu wenye ulemavu linajumuishwa kwenye mchakato wa mabadiliko ya katika mpya kwa ajili ya kupata mawazo ya pande zote.

Alisema maoni hayo yatasaidia mahitaji maalum ya kundi hilo kutambuliwa kikatiba kama makundi mengine kwenye jamii.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa kongamano pamoja na Taasisi ya Kusaidia Watu Wenye Ulemavu ya Mbunge wa Viti Maalum, Khadija Taya, maarufu Keysha iitwayo Keysha Empowerment Development Foundation (KEDEF) jana, alisema serikali inatambua kundi la watu wenye ulemavu litahitaji utaratibu maalum kutokana na utofauti na aina mbalimbali za ulemavu na mahitaji tofauti yaliyopo katika kundi hilo.

"Kuhusu hoja ya watu wenye ulemavu kujumuishwa katika mchakato wa mabadiliko ya Katiba ni kutokana na kuwa na changamoto nyingi na tofauti zao," alisema na kuongeza:

"Pia ni nyingi na pengine hili ni kundi maalum na linahitaji utaratibu maalum kwa kila ngazi, serikali itahakikisha watu wenye ulemavu wanapewa fursa stahiki katika majukwaa mbalimbali kama wengine, utaratibu utakaowekwa hamtakosa nafasi kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inayoratibu shughuli za serikali maadam mmelileta tutalisimamia kikamilifu," alisema.

Kuhusu mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa watu wenye ulemavu ya mwaka 2004 alisema serikali imetenga fedha kiasi cha Sh. milioni 135, kwa ajili ya kuanza kufanya tathmini ya utekelezaji wa sera na maandalizi ya mkakati na utekelezaji wake na kuwaahidi kuwa watashirikishwa vyema katika mapitio hayo ya kubadilisha sera ili kupata mpya na kutungiwa sheria mpya zitakazoendana na mahitaji yao ya sasa.

Waziri Mkuu pia aliahidi serikali kuendelea kuwakumbuka watu wenye ulemavu katika nafasi mbalimbali za ajira serikalini kama ilivyokuwa ikifanya na kutoa mfano wa baadhi yao ambao tayari wameajiriwa serikalini, ikiwamo makatibu wa wakuu na manaibu makatibu wakuu katika wizara mbalimbali akiwamo pia aliyekuwa Mwenyekiti wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu, Ummy Nderianaga ambaye kwa sasa ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu).

Mwenyekiti wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Ernest Kimaya, alitaja changamoto mbalimbali zinazowakumba watu wenye ulemavu, ikiwamo gharama za ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kutumiwa na kundi hilo akiomba serikali kutoa punguzo la kodi katika vifaa hivyo, ili kushusha bei ya vifaa hivyo wamudu kuvipata kwa urahisi.

Mbunge Keysha alisema lengo lake ni kutoa elimu kuhusu haki mbalimbali zinazopatikana kwa mujibu wa sheria kuhusu huduma za watu wenye ulemavu, pia kulijengea uwezo kundi hilo ili nafasi mbalimbali za ajira zinapotoka wawe na sifa za kuzipata. Aliishukuru serikali kwa kuwa bega kwa bega kwa kuwasikiliza na kutekeleza mahitaji yao.

Alitoa mfano wa Sheria ya Ununuzi ambayo inataka asilimia 30 ya ununuzi wa umma itengwe kwa ajili ya kundi hilo akitaka uwekwe mwongozo katika taasisi zote kutambua na kupeleka mrejesho katika Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu utekelezaji wake.

# Aomba msaada kupata ndugu wa marehemu

**Na Halfani Chusi**

MKUU wa Utawala Kampuni ya Ulinzi ya JFM Security, Meck Peter, amewaomba Watanzania kusaidia kuwapata ndugu wa aliyekuwa mlinzi wake, Didas Majala aliyeugua ghafla na kufariki dunia akiwa anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala, Dar es Salaam.

Mwishoni mwa wiki, Peter aliiambia Nipashe kuwa ni zaidi ya siku ya 10 tangu mfanyakazi wake huyo kufariki dunia, lakini mazishi hayajafanyika kutokana na ndugu zake kutopatikana na kutoa rukhsa ya kuzika mwili.

Alisema wakati anaajiriwa aliacha namba za wadhamini wake ambao ni Roberty Rocky lakini kila alipojaribu kuwatafuta walikokuwa wanaishi na kuwapigia simu hawakupatikana.

"Nimekwenda polisi, nimeshatoa taarifa, nimewatafuta ndugu zake kwa kutumia namba za simu zilizopo kwenye mkataba wa ajira, wote hawapatikani.

Ninaomba yeyote anayewafahamu ndugu zake atoe taarifa katika Hospitali ya Mwananyamala au kwa kupiga simu namba 0712498854.

"Ili tuweze kukutana na ndugu zake, tuwape taarifa ya kile kilichotokea hadi umauti ulipomfika, kwa sababu anapoendelea kukaa mochwari gharama inazidi kuongezeka na kiimani mwili unapokaa muda mrefu maiti inapata maumivu," alisema.


**IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 85 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the LATE IDDI SONGORO MZUGU**
**BY**
**GEOFREY JOSEPH MZUGU**
**JAMES JOSEPH MZUGU......PETITIONERS**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 21 day of 8..............2023
Dated at Dodoma this 27 day of 07...........2023

Presented for filling this 08/05/2020

RESIDENT MAGISTRATE

**DODOMA**



TRA

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

## TAARIFA KWA UMMA

### UTARATIBU WA ULIPAJI WA KODI YA ZUIO YA ASILIMIA MBILI (2%) KWENYE MALIPO YA UNUNUZI WA MADINI

Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 imefanya marekebisho ya kifungu cha 83(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Na. 332, Toleo la Mwaka, 2019 kwa kuanzisha wajibu wa kuzuia kodi ya mapato ya **asilimia mbili (2%)** kwenye malipo yanayohusika na ununuzi wa madini ya metali yenye thamani, madini ya vito na mawe ya vito (precious metals, gemstones and other precious stones), pindi yatakapouzwa na mchimbaji mdogo mwenye leseni na asiye na leseni. Utekelezaji wa mabadiliko haya ya sheria umeanza tangu tarehe **1 Julai, 2023.**

Kulingana na marekebisho yaliyofanyika kwenye sheria tajwa, mlipaji wa kodi ni Mchimbaji mdogo mwenye leseni au asiye na leseni. Ili kuwasilisha kodi hiyo TRA, Mfanyabiashara mdogo wa biashara ya madini (Broker) atazuia kodi wakati anafanya malipo kwenda kwa Mchimbaji kutokana na ununuzi wa madini ambao ataufanya kwenye vituo vya ununuzi wa madini (buying centers). Aidha, mfanyabiashara huyo mdogo (Broker) atakapouza madini yake kwenda kwa mfanyabiashara mkubwa (Dealer), hatakatwa kodi ya zuio.

Vilevile, pale ambapo Mchimbaji mdogo mwenye leseni au asiye na leseni atakapouza madini yake kwenda kwa Mfanyabiashara mkubwa wa biashara ya madini (Dealer), mfanyabiashara huyo atazuia kodi wakati wa kufanya malipo kwa mchimbaji kwenye Soko la Madini (Mineral markets) na kuiwasilisha kodi hiyo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Ifahamike ya kwamba kodi itakayozuiwa na Mfanyabiashara wa biashara ya madini itakuwa ni kodi ya mwisho kwa mchimbaji wa madini kama ilivyobainishwa kwenye Kifungu cha 86(1)(g) cha Sheria ya Kodi ya Mapato. Hii inamaanisha kwamba, mchimbaji mdogo mwenye leseni au asiye na leseni hatawajibika tena kukadiriwa au kujikadiria kodi kwenye mapato ambayo **chanzo chake ni uuzaji wa madini tajwa hapo juu**.

Tunapenda kuwajulisha kwamba Maafisa wa TRA watakuwepo kwenye Masoko ya Uuzaji wa Madini ili kutoa huduma zitakazowezesha ulipaji wa kodi hiyo pamoja na kutoa ufafanuzi wa masuala ya kodi utakaohitajika.

Wafanyabiashara wadogo wa biashara ya Madini (Brokers) wanasisitizwa kuwa, pindi wanapofika kwenye masoko ya madini wahakikishe wanakuja na majina na Namba za Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) ya Wachimbaji wadogo wa madini ambao wamewakata kodi, ili kuwezesha kodi itakayokatwa iweze kuakisi kwenye TIN ya Mchimbaji husika badala ya Mfanyabishara wa madini (Broker/Dealer).

Wachimbaji wadogo ambao hawana TIN, huduma hiyo itatolewa kupitia Vituo na Masoko ya madini pamoja na Ofisi za Kodi za Mkoa. Kwa mawasiliano zaidi, tafadhali tembelea Ofisi ya TRA iliyo karibu nawe au tumia anwani zifuatazo kuwasiliana nasi :-

| | |
|---|---|
| Tovuti | : **www.tra.go.tz** |
| Namba za Bure za Kupiga | : **0800 750 075** au **0800 780 078** au **0800 110016** |
| WhatsApp | : **0744 23 33 33** |
| Barua Pepe | : **huduma@tra.go.tz** |

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;

A.J. Kidata
**Kamishna Mkuu**

# Hatima kesi mkataba wa DP World leo

**Na Kulwa Mzee,** MBEYA

MACHO na masikio ya Watanzania leo yanatarajiwa kuelekezwa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya katika kesi ya kupinga mkataba wa uwekezaji, kuendesha na kuendeleza bandari nchini.

Uamuzi huo unatarajia kutolewa mbele ya jopo la majaji watatu, Jaji Dunstan Ndunguru, Jaji Mustafa Ismail na Jaji Abdi Kagomba waliosikiliza shauri hilo.

Shauri hilo lilifunguliwa na Watanzania wanne kutoka mikoa tofauti; Alphonce Lusako, Emmanuel Chengula, Raphael Ngonde na Frank Nyalus dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Katibu wa Bunge la Tanzania, ambaye ni Mtendaji Mkuu na Mratibu wa Shughuli za Bunge.

Walalamikaji wanawakilishwa na Mawakili Mpale Mpoki, Boniface Mwabukusi, Livino Ngalimitumba na Philipo Mwakilima.

Pande zote mbili katika shauri hilo zilikubaliana kwamba hoja sita ndizo zinazobishaniwa mahakamani; ya kwanza ni kama kutia saini, kuwasilisha bungeni na kuridhia mkataba wa Tanzania na Dubai kulikiuka kifungu cha 11(2), Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Raslimali na Maliasili, Sheria Na. 5 ya Mwaka 2017 kikisomwa pamoja na Sheria ya Mapitio na Majadiliano ya Mikataba ya Masharti Hasi, Sheria Na. 6 ya Mwaka 2017.

Hoja ya pili ni kama umma uliarifiwa na kupewa muda mwafaka kushiriki na kutoa maoni yao kama sheria zinavyotaka kuhusiana na utaratibu wa kupitisha na kuridhia mikataba.

Katika shauri hilo, hoja ya tatu ni kama ibara ya 2, 4(2) zinakiuka Ibara namba 1,8 na hoja ya nne, kama IGA kati ya Tanzania na Dubai ni mkataba na hoja ya tano kama Ibara ya 2 na 23 za IGA zinakiuka kifungu cha 25 cha Sheria za Mikataba Tanzania.

Hoja ya sita inayobishaniwa ni kama IGA kati ya Tanzania na Dubai ilifuata taratibu za kisheria katika kuchagua njia ya zabuni ambazo zimewekwa chini ya kifungu cha 64 cha Sheria ya Ununuzi.

Kiongozi wa jopo la mawakili wa serikali, Wakili wa Serikali Mkuu, Mark Mlwambo awali aliweka pingamizi dhidi ya shauri hilo, akiomba mahakama itupilie mbali. Alitoa sababu nne, lakini Julai 25 mwaka huu upande wa serikali uliamua kuondoa pingamizi.

Wakili Mlwambo akiwasilisha hoja za kuomba kuondoa pingamizi akidai sababu kubwa ni kupisha usikilizwaji wa shauri mama na hakuna gharama kwa upande wowote.

Wakili Mpale Mpoki, akiwawakilisha walalamikaji, alikubaliana na hoja ya serikali kuondoa pingamizi, pia walijadiliana na wateja wao ambapo nao walikubaliana wakiwa na lengo la kuharakisha usikilizwaji na uamuzi wa shauri la msingi.

Walalamikaji katika shauri hilo wanapinga makubaliano yanayohusisha uwekezaji katika bandari za Tanzania zilizoko katika mwambao wa bahari na katika maziwa, kuwa ni batili kwa kuwa yana ibara zinazokiuka sheria na Katiba ya nchi.

Wanadai makubaliano hayo yanahatarisha mamlaka ya nchi na usalama wa taifa na yaliridhiwa na Bunge kinyume cha utaratibu bila kuwapa nafasi ya kutosha wananchi kutoa maoni yao.

Makubaliano hayo yalitiwa saini Oktoba 25, 2022 na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, baada ya kupewa nguvu ya kisheria na Rais Samia Suluhu Hassan, huku Katibu Mkuu wa wizara hiyo, akishuhudia na yaliridhiwa na Bunge Juni 10, 2023.

Kesi hiyo ilianza kusikilizwa Julai 25 mpaka Julai 28 mwaka huu, mawakili wa waombaji katika shauri hilo walipomaliza kuwasilisha hoja zao huku wakidai mkataba umekiuka sheria na Katiba ya nchi.



Mwanafunzi Gift Ally wa Shule ya Sekondari King'ongo, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, akichangia mada katika mafunzo ya uongozi yaliyoandaliwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kata ya Saranga kwa uratibu wa Mtandao wa Jinsia Tanzania TGNP juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Walimu 2, mchapishaji mbaroni kughushi vyeti

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

WALIMU wawili na mchapishaji wamefikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita, wakikabiliwa na makosa matano ya kughushi vyeti vya kifo, ndoa, kuzaliwa na kadi ya Bima ya Afya (NHIF), vitendo ambavyo ni kinyume cha sheria.

Washtakiwa hao ni Maria Salome (56) mchapishaji binafsi, Jilala Charles (34), Mwalimu wa Shule ya Msingi Ibozyamagigo na Matatizo Mkosa (31), Mwalimu wa Shule ya Msingi Lwenge.

Washtakiwa wote kwa pamoja walipandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa mahakama hiyo, Johari Kijuwile na kukana kuhusika na makosa yote matano.

Washtakiwa wawili walipata dhamana na mmoja alipelekwa mahabusu kwa kukosa dhamana.

Aliwataja washtakiwa waliotimiza masharti ya dhamana kuwa ni Salome na Charles na ambaye hakutimiza masharti ni Mkosa aliyepelekwa mahabusu Gereza la Wilaya ya Geita.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Venance Mkonongo, ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya washtakiwa kusomewa maelezo ya awali pamoja na kuanza kusikiliza mashahidi wa upande wa Jamhuri.

Hakimu alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Agosti 16, mwaka huu, kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa hao maelezo ya awali na kusikiliza mashahidi wa upande wa Jamhuri.

Akisoma hati ya Mashtaka Wakili wa Serikali Mkonongo, alidai kosa la kwanza linalowakabili washtakiwa wote watatu ni kwamba Novemba 26 mwaka 2022, maeneo ya Mtaa wa Msalala, Mkoa wa Geita, washtakiwa wote walighushi cheti cha ndoa cha Mkosa na Gwatoye, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Alidai kosa la pili linamkabili mshtakiwa wa kwanza Salome, terehe isiyojulikana Novemba mwaka 2022 mshtakiwa huyo alighushi cheti cha kifo cha Mashauri, cha kuzaliwa cha Kihengu Chacha na Tusumege Alex kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Pia alidai kosa la tano linawakabili washtakiwa wawili Jilala na Matatizo ambao wanadaiwa kwa nyakati tofauti kwenye maeneo ya Ofisi ya Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF), Mkoa wa Geita waliwasilisha cheti cha ndoa kilichoghushiwa chenye majina ya Mkosa na Gwantoye kwa lengo la kujipatia kadi ya NHIF, jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

# Waziri Mkuu aiagiza TADB kufungua matawi zaidi Nyanda za Juu Kusini

**Na Salome Kitomari**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), kufungua matawi zaidi Nyanda za Juu Kusini, ili kufikisha huduma kwa wakulima wengi zaidi na kuleta mabadiliko makubwa ya kilimo.

Kiongozi huyo alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki baada ya kutembelea banda la Benki ya TADB katika maonesho ya Nanenane yanayoendelea katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.

Aliipongeza TADB kwa kazi nzuri ya kutoa mikopo yenye riba nafuu zaidi na kuitaka kufungua matawi zaidi katika mikoa ya Iringa, Ruvuma na Rukwa kwa kuwa maeneo hayo yana wakulima wengi ambao wangependa kufikiwa na huduma hizo.

Kaimu Mkurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti wa benki hiyo, Mkani Waziri, alisema wanatoa mikopo na faida kwa makundi yote ya vijana na wanawake kwa lengo la kuhakikisha ushiriki wao kikamilifu katika shughuli za kilimo.

Mkani alimweleza Waziri Mkuu kuwa tangu benki hiyo ianze kufanya kazi hadi kufikia hivi sasa, imeshatoa mikopo ya kilimo yenye thamani ya Sh. bilioni 608.5 iliyonufaisha wakopaji 1,657,544.

Alisema TADB inawafikia wakulima katika kada mbalimbali ikiwamo wakulima wadogo.

Waziri Mkuu pia alielekeza TADB kuandaa mikakati ya kushawishi taasisi zingine za kifedha, zikiwamo benki za kibiashara kushusha riba chini.

Katika ziara yake katika banda la TADB Majaliwa pia alipata nafasi ya kuona kazi za wanufaika wa TADB ikiwamo TANICA coffee (Kagera) katika sekta ya kahawa, na JND Polybags Company (kutoka Iringa) - watengenezaji wa mifuko ya kuhifadhi nafaka.

TANGAZO

# SHIFA PAN AFRICAN HOSPITALS LTD.

Plot 30-31, Msese Road, Kinondoni, P. O. Box 20417, Dar-es-Salaam




WE ARE HIRING!

## ARE YOU READY TO JOIN AN AMBITIOUS TEAM TO TRANSFORM HEALTHCARE IN TANZANIA?

**Shifa Pan African Hospitals (SPAH) is a 250 bed tertiary care hospital located in Dar-es-Salaam, Tanzania. With state of the art medical equipment, robust infrastructure, adherence to international medical standards and experienced medical staff, SPAH's vision is to provide the highest quality medical care in Africa. We are now seeking a pool of qualified, experienced and progressive medical staff to join us in this vision.**

### CONSULTANTS / ASSOCIATE CONSULTANTS / MEDICAL OFFICERS

• Internal Medicine • Cardiology • Ophthalmology • OBS/GYN • Nephrology
• Pulmonology • Urology • Anesthesia • Radiology • Pathology
• Pediatrics • Gastroenterology • ENT • Emergency Medicine
• General Surgery • Orthopedics • Endocrinology • Dental

### NURSING / TECHNOLOGISTS / TECHNICIANS

• Critical Care Nurse • Staff Nurse • Pediatric Nurse • LHV/Midwife
• Lab Technologist • Dialysis Technologist • Radio Technician
• Dialysis Technician • Lab Technician • Anesthesia Technician
• CSSD Technician • OR Technician • Pharmacist • Perfusionist

## APPLY NOW!

Please send your updated resumes at **hr@spah-tz.com** latest by 20-August-2023.
Please clearly mark the position applied for in the subject field of the email.

* SPAH offers equal opportunity employment along with a high capacity building environment and market competitive benefits.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Rekodi kujaza uwanja siku 3 kabla isiishie Simba Day

**SIMBA** imekuwa klabu ya kwanza ya soka nchini kuweka rekodi ya kununua tiketi zote 60,000 za kuujaza Uwanja wa Benjamin Mkapa siku tatu kabla ya tamasha lao la kila mwaka la Simba Day.

Tamasha hilo ambalo hutumiwa kutambulisha wachezaji wao wa msimu mpya huambatana na burudani mbalimbali pamoja na mchezo maalum wa kirafiki, lilifanyika jana, Jumapili kwa kuhitimishwa na mchezo dhidi ya Power Dynamos FC ya Zambia.

Simba ambao ndio waasisi wa matamasha hayo nchini, hilo ni tamasha lake la 15, tangu kuyaasisi mwaka 2009 na ndipo baadhi ya klabu zikaiga utamaduni huo kila moja ikilitambulisha kwa jina lake.

Klabu zingine zilizofuata kwa kuanza kufanya tamasha kama hilo, ni Yanga likitambulika kama Siku ya Mwananchi, kisha Azam FC likijulikana kama AZAMKA, ambayo hata hivyo msimu huu imeshindwa kulifanya.

Lakini Namungo nayo imewahi kufanya, Biashara United pia ikija na Biashara Day pamoja na wiki iliyopita klabu iliyopanda daraja na kutisha msimu uliopita, Singida Fountain Gate FC nayo ilikuja na tamasha lake likijulikana kama Singida Day.

Hata hivyo, pamoja na ukongwe wa Simba kwenye matamasha hayo na klabu zingine zilizofuata, hakuna klabu hata moja iliyowahi kuuza tiketi za kuujaza uwanja wake zikaisha siku tatu kabla ya tukio ama hata mechi husika.

Hii ni rekodi ya kuvutia na yakukumbukwa kwa soka la Tanzania kwani licha ya baadhi ya mechi nyingi kuchezwa nchini na kuvutia mashabiki wengi na uwanja kujaa, tiketi nyingi huuzwa siku ya mchezo tena dakika za mwisho.

Hali kama hiyo ya Simba imezoeleka Ulaya kwani mashabiki mara nyingi hununua tiketi za msimu mzima ama miezi mitatu kabla ya mechi husika. Hivyo mashabiki wa Simba kununua tiketi zote 60,000 siku tatu kabla ya mechi ni suala la kupongezwa sana na kutakiwa kuigwa na mashabiki wote wa soka nchini.


Tukiwa wadau wa soka namba moja nchini, tunatamani na kuhamasisha mashabiki wote wa soka kuelekea msimu ujao unaotarajiwa kuanza Agosti 15, mwaka huu, kuiga mfano huo wa kununua tiketi mapema na wale wa Simba tukiwataka usiishie hapo bali uwe endelevu.

Kuna faida nyingi chanya kwa mashabiki kununua tiketi mapema, kwanza ni kuondoa usumbufu wa kuhangaika kwenye foleni siku ya mechi, lakini pia kuwa na uhakika wa kuingia uwanjani na klabu kuweza kuwa na takwimu sahihi za mapato yake mapema.

Aidha, ni wakati sasa kwa kila shabiki wa soka kuendelea kujitokeza uwanjani kuzisapoti timu zao kufanya vizuri kuelekea msimu mpya na si tu kuishia kwenye matamasha kama haya na wengine kuacha utamaduni wao wa kuchagua baadhi ya mechi za kwenda kutazama.

Matarajio yetu pia ni kuona kwa mechi zile wanazoziita ndogo za Ligi Kuu Bara, angalau mashabiki wakijitokeza hata nusu ya Uwanja wa Mkapa ili kuifanya Ligi Kuu Bara kuendelea kuwa sehemu sahihi kwa wanasoka wengi wakubwa kutoka nje kutamani kuja kucheza, lakini ikizidi kupanda katika viwango vya Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Ratiba Ligi Kuu isiziumize wala kuzidekeza za michuano CAF

Na Adam Fungamwango

**WAKATI** wowote kuanzia leo, Bodi ya Ligi nchini (TPLB), inaweza kutoa ratiba ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa 2023/24.

Awali, bodi hiyo kupitia kwa Ofisa Mtendaji Mkuu, Almasi Kasongo, alisema wamechelewa kutoa ratiba hiyo kutokana na kuisubiria ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), kwanza ndipo nao waweze kutengeneza yao kuzikwepesha timu zinazocheza kimataifa.

Ratiba ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho imeshatoka, imesalia ya African Football League (Super Cup), ambayo Simba inashiriki na kufuzu kwa michuano ya Kombe la Dunia na AFCON.

Wakati wadau na mashabiki wa soka wanasubiria ratiba hiyo, binafsi nataraji itatoka ya haki bila kuziumiza au kuzibeba timu zote zinazoshiriki michuano ya kimataifa.

Simba na Yanga zitacheza Ligi ya Mabingwa huku Azam FC pamoja na Singida Fountain Gate, zenyewe zikicheza Kombe la Shirikisho Afrika.

Napenda kuipongeza TPLB kwani kwa misimu mwili iliyopita hakukuwa na malalamiko sana kwenye upangaji wa ratiba kuingiliana na mechi ya kimataifa, lakini kuacha viporo vingi.

Nakumbuka miaka ya nyuma, Simba au Yanga ikiwa na mechi za kimataifa inakuwa na viporo vinavyofika mpaka mechi saba, kitu ambacho hakitoi haki kwa timu zingine.

Miaka miwili iliyopita pamoja na wingi wa timu zinazoshiriki, lakini ratiba imekuwa rafiki zaidi kiasi kwamba timu inayoshiriki kimataifa inaweza kuwa na kiporo kimoja au viwili tu.

Wakati mwingine timu zinazocheza kimataifa zinaanza kwanza kucheza mechi ya ligi raundi inayofuata kabla ya zingine, halafu zinasafiri huku nyuma zinazobaki zinakuja kukamilisha baadaye.

Kwa hili Bodi ya Ligi inastahili pongezi kwa sababu wamelipunguza kwa kiasi kikubwa. Bado kuna tatizo dogo la baadhi ya klabu kuomba kuahirishiwa mechi kwa sababu ya mechi hizo za kimataifa.

Kwa mustakabali wa soka la nchi yetu ni muhimu sana kwa wasimamizi wa soka kuipa timu yoyote msaada na upendeleo maalum wa hali na mali kama jambo hilo kuna manufaa kwa klabu au timu ya taifa, lakini kuna mengine inabidi Bodi iyaangalie mara mbilimbili.

Kuna klabu inaweza kuomba iahirishiwe mechi ya ligi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya kimataifa kwa wiki mbili. Bodi ya Ligi isikubali suala hili na hata kwenye ratiba ijaribu kuweka angalau siku tano au saba timu kutoka kucheza mechi ya ligi kwenda kimataifa au kinyume chake.

Kupumzika kwa zaidi ya wiki baadhi ya viongozi na makocha wanadhani wanawapumzisha wachezaji wao kumbe ndiyo wanasababisha kukosa utimamu wa mwili wa mechi husika 'match fitness.'

Hiyo imeshawahi kutokea wakati Simba ikienda kucheza mechi ya kwanza ya robo fainali dhidi ya Kaizee Chiefs nchini Afrika Kusini ambapo ilipewa wiki mbili kujiandaa, ikachapwa mabao 4-0, lakini baada ya kucheza mechi ya huko, siku chache baadaye ikashinda mabao 3-0 nchini.

Moja ya sababu kubwa iliyotajwa ni wachezaji kukaa muda mrefu bila kucheza. Hili lisirudiwe tena na TPLB isiogope lawama kutoka kwa viongozi wa klabu hizo.

Ratiba ipangwe bila kuziumiza kuzipa mechi moja kabla hazijasafiri, lakini pia bila kuzidekeza kwa kuzipa wiki mbili kujiandaa. Mimi nadhani siku tano au wiki zinafaa sana kutoka kucheza mechi moja hadi nyingine, iwe ya ligi kwenda kimataifa au kimataifa kurudi kucheza ligi.

TANGAZO

# Mchango wa JICA katika kuendeleza kilimo Tanzania

Jafari Juma, Mwananchi

**Ushirikiano wa JICA na Tanzania katika sekta ya kilimo**

Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA) linaadhimisha zaidi ya miaka 60 ya shughuli zake za ushirikiano na Tanzania. JICA inaungana na wananchi wa Tanzania kuadhimisha Siku ya Wakulima yaani "Nanenane" Agosti 8, 2023, kwa kueleza historia yake katika kusaidia maendeleo ya Tanzania katika sekta ya kilimo.



Timu ya kilimo ya JICA Tanzania

JICA imekuwa ikihimiza uboreshaji wa uzalishaji, biashara na uanzishaji wa viwanda katika sekta ya kilimo ili kuendana na vipaumbele vya nchi, hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi wa Tanzania na maendeleo ya jamii.

JICA imetoa misaada nchi nzima kupitia programu kuu mbili, "Programu ya kuimarisha uzalishaji wa mpunga" na "Programu ya kukuza kilimo kibiashara/viwanda". Misaada hiyo ambayo ilianza tangu miaka ya 1970 imekuwa msingi wa maendeleo ya kilimo Tanzania kama vile kilimo cha mpunga, uendelezaji wa umwagiliaji, kuimarisha mfumo wa nchi na kadhalika.

**TANSHEP sasa inajumuishwa katika mipango ya Serikali na mifumo ya maendeleo ya kilimo**

Mradi wa Tanzania SHEP (Smallholder Horticulture Empowerment & Promotion) unaotekelezwa na Wizara ya Kilimo (MoA) na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kwa kushirikiana na JICA, umekuwa ukibadilisha fikra za wakulima kutoka "Kuzalisha na Kuuza". mpaka "Kuzalisha ili kuuza" ili kuzalisha kwa ajili ya biashara na kuboresha mapato yao.



Vijana wa BBT wakifanya utafiti wa masoko chini ya msaada wa kiufundi wa TANSHEP.

Utafiti uliofanywa unaonyesha kuwa wanufaika (wakulima) wameongeza mapato yao kwa asilimia 45 kupitia mfululizo wa mafunzo ya kiufundi. Wakulima hufanya utafiti wa soko kabla ya kuanza kulima ili kuamua ni zao gani watazalisha na jinsi/lini kama kanuni ya SHEP inavyoeleza.

Kutokana na ufanisi na umuhimu wake, mbinu ya SHEP imepitishwa katika mikakati na programu mbalimbali za Serikali ikiwa ni pamoja na 'Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Kilimo cha mbogamboga na matunda' na 'Mpango Kazi2021-2031' ambao ulipitisha mbinu hiyo kama afua muhimu ya kuboresha masoko na upatikanaji wa masoko. Kwa sasa inatekelezwa na mpango wa "Building a Better Tomorrow (BBT) wenye lengo la kuimarisha uwezo wa vijana na wanawake kwa ajili ya kilimo biashara.

SHEP pia imejumuishwa katika mtaala wa mafunzo katika vyuo vya mafunzo vya Wizara ya Kilimo (MATIs), ambapo wanafunzi wanafundishwa kuwa maafisa ugani wa kitaaluma wa siku zijazo. Katika ngazi ya mashambani, Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa sasa zinasambaza mbinu ya SHEP kwa vikundi mbalimbali vya wakulima kwa juhudi zao wenyewe kwa kuwatumia maafisa ugani waliopewa mafunzo na mpango wa TANSHEP. Kauli mbiu ya TANSHEP ambayo ni "Anzia Sokoni, Malizia Shambani, Kwa Kipato Zaidi", sasa inasikika vyema sio tu kutoka kwa wanufaika wa TANSHEP bali pia kwa wakulima, wanafunzi, maafisa ugani na watu wengine.

**Mradi wa mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani milion 70 kwa ajili ya kuboresha na kuendeleza uzalishaji wa chakula**

Ili kuendana na ajenda ya kitaifa ya kilimo ambayo inalenga kufikia zaidi ya asilimia 10 ya ukuaji wa sekta ya kilimo ili kuhakikisha usalama wa chakula na usambazaji kwa mahitaji ya ndani na nje ya nchi ifikapo mwaka 2030, JICA pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) wanatekeleza "Mradi wa Kusaidia Pembejeo za Kilimo Tanzania (TAISP)". Mradi wa mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 70 utahakikisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo hasa mbegu bora na mbolea inayolenga kuboresha uzalishaji, kuongeza tija na faida ya mazao ya kipaumbele.




Mradi wa kuwezesha upatikanaji wa pembejeo za kilimo Tanzania.

Mazao yanayolengwa ni ngano, alizeti na mpunga ili kuongeza kasi ya utoaji wa pembejeo za bei nafuu (mbegu zilizoidhinishwa na mbolea) kwa wakulima wadogo katika maeneo yaliyolengwa (Arusha, Manyara, Mbeya, Rukwa, Kilimanjaro, Njombe, Singida, Dodoma, Morogoro) Songwe, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Geita). Makadirio ya jumla ya wanufaika wa moja kwa moja ni kaya 1,200,000, sawa na watu 4,800,000, ambapo asilimia 40 ni wanawake na vijana.

**Mtaalamu wa fedha kushirikiana na TADB kwa ajili ya kuendeleza kilimo**

Ili kutekeleza juhudi za nchi katika kuimarisha upatikanaji wa fedha za kilimo ili kuimarisha minyororo ya thamani ya chakula, JICA imemleta Mtaalam, Bw. Takayuki Urade, kusaidia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa kimsingi katika taasisi za fedha, kama vile kutambua na kuandaa miradi ya uwekezaji/mikopo, tathmini ya mikopo, usimamizi wa viashiria hatarishi, ufuatiliaji wa uwekezaji/mikopo, kuboresha upatikanaji wa fedha kwa wakulima, uimarishaji wa mikopo kwa benki za sekta binafsi n.k. Muda wake wa kazi utaendelea hadi Februari 2024.

**Kwa ushirikiano wa muda mrefu katika maendeleo ya zao la mpunga, mradi mpya wa ushirikiano waanzishwa**

Juni 2023, JICA kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo ilianza rasmi "Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Wadau wa Maendeleo ya Sekta ya Mpunga katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania" (TANRICE 3) unaotekelezwa kwa miaka mitano hadi 2028.

Tanzania imeweka mpunga kama zao la kipaumbele na la kimkakati kwa maendeleo ya kilimo kwa uhakika wa chakula na mapato kwa wakulima wa vijijini.

JICA imekuwa ikiisaidia Tanzania kuboresha sekta ya kilimo kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na teknolojia ya kilimo cha umwagiliaji mpunga katika Mkoa wa Kilimanjaro tangu miaka ya 1970, kuanzisha na kuimarisha utendaji kazi wa Kituo cha Mafunzo ya Kilimo Kilimanjaro (KATC), kuanzisha mfumo wa kilimo cha mpunga na mbinu za mafunzo zinazofaa kwa mashamba ya wakulima na tangu mwaka 2007 kupitia TANRICE1 na TANRICE2, JICA imekuwa ikitoa mafunzo ya kitaalamu ya kilimo cha mpunga nchi nzima na imesaidia jumla ya wakulima 44,000, hasa katika maeneo ya umwagiliaji.

Kutokana na hali hiyo, tija ya wakulima katika maeneo yaliyolengwa imeongezeka kutoka t/ha 3.2 hadi 4.5 t/ha.

Pamoja na mafunzo ya teknolojia ya kilimo cha umwagiliaji mpunga, TANRICE 3 itafanya kazi ya kuboresha tija katika maeneo ya uzalishaji wa mpunga unaotegemea mvua, ambayo ndiyo sehemu kubwa ya uzalishaji wa mpunga nchini Tanzania.

Inatarajiwa kwamba idadi ya wakulima wanaotumia mbinu za uzalishaji wa mpunga zilizopendekezwa na mradi huu itaongezeka na kwamba ongezeko la mavuno ya mpunga litasababisha ongezeko la uzalishaji wake nchini Tanzania.

**AFICAT kwa teknolojia za kisasa na zana za kilimo nchini Tanzania**

Wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Tokyo kwa Maendeleo ya Afrika (TICAD 7) uliofanyika Yokohama, Japan, mwaka 2019, Kituo cha Ubunifu wa Teknolojia za Kilimo Afrika (AFICAT) kilipendekezwa kuanzishwa katika nchi za Afrika kwa ajili ya kukuza teknolojia na zana za kilimo kupitia ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi kati ya Japan na nchi za Afrika.

Tangu Machi 2022, JICA imekuwa ikituma timu ya wataalamu wa Japani kuja Tanzania kuendesha AFICAT kama shughuli za majaribio kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na wadau wengine kwa kualika kampuni, bidhaa na teknolojia za Japani. Hadi sasa, AFICAT inafanya kazi na kampuni zaidi ya 10 za kilimo za Japani kwa shughuli zake kama vile maonyesho kwa wakulima na viongozi wa Serikali na uhakiki wa mashamba ya KATC, ambayo ni msingi wa uendeshaji wa AFICAT pamoja na kuthibitisha bidhaa zao.

Kampuni hizo ni pamoja na Honda Motor Co., Ltd. (power tiller, water pump, backpack sprayer na brush cutter), Matsuyama Plow MFG. Co., Ltd. (vifaa vilivyopewa jina drive harrow), Kett Electric Laboratory Co. Ltd. (grain moisture testers na whiteness tester), Bando Chemical Industries, Ltd. (mikanda ya mashine za kilimo), Japan Conservation Engineers & Co., Ltd. ("Fujimin", msaidizi wa ukuzaji mimea), na Pulsar International Corporation ("Orgamin", mbolea ya asili ya majani) wamekuwa wakifanya semina za mtandaoni na uthibitishaji wa mashamba ndani na nje ya KATC kwa kutumia bidhaa zao zilizonunuliwa kutoka Japani. Timu ya AFICAT itaendelea kufanya kazi za majaribio nchini Tanzania hadi mwisho wa mwaka 2023.



Uthibitishaji wa aina mpya ya bidhaa za Matsuyama KATC.

**Kuelekea utekelezaji wa maendeleo ya kina ya umwagiliaji**

Kwa kuwa Serikali ya Tanzania imeweka kipaumbele katika maendeleo ya umwagiliaji, pamoja na Tume ya Kitaifa ya Umwagiliaji (NIRC), JICA ilisaidia kuandaa miongozo ya maendeleo ya skimu za umwagiliaji pamoja na kutoa msaada wa kifedha kwa kuandaa mpango kabambe wa umwagiliaji.


Ili kuongeza uwezo wa maafisa wa NIRC katika kutekeleza uendelezaji wa umwagiliaji kulingana na mwongozo huu, JICA imetoa mafunzo kwa maafisa hao kwa zaidi ya miaka 10 tangu 2010 na inapanga kutuma mshauri katika eneo hilo.

**Kukuza ushirikiano na sekta binafsi**

JICA pia inalenga kusaidia maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Tanzania kwa kutumia uzoefu na ujuzi wa kampuni binafsi za Japan. Kwa sasa, JICA ina ushirikiano na kampuni tano za Kijapani zinazohusiana na kilimo/sekta ya chakula kama vile Nisshin honey CO., LTD., KAWAKAMI MOKUZAI Co., LTD., SATAKE Cooperation, Kikkoman Corporation na Kagla Vaportech Corp.



Mtindo wa kisasa wa ufugaji nyuki wa Nisshin honey Co, Ltd una jukumu muhimu katika kuongeza kiwango cha asali hadi mara nne zaidi ya njia za asili.




SATAKE Cooperation ilitambua mahitaji makubwa ya mashine za kuchambua mazao kupitia utafiti na maonyesho.



Kampuni ya chakula ya Kijapani ya Kikkoman inafanya kazi na JICA kukuza teknolojia ya uandaaji wa vyakula vya nafaka nchini Tanzania na kuifanya iwe rahisi kupika vyakula vya soya vyenye protini nyumbani.



Kawakami Mokuzai (uhandisi wa mbao) huleta mbinu za uhandisi kwa uzalishaji wa mizinga ya kisasa ya mbao nchini Tanzania.



Mfumo wa gesi ya LP wa Kagla Vaportech Corp, unachangia katika upishi safi.

# Watilia mkazo uendelezaji wa wahandisi wanawake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMPUNI ya AngloGold Ashanti - Geita Gold Mining Limited (GGML), imeahidi kushirikiana na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuongeza ushiriki wa wanawake katika maendeleo ya nchi kwa kuwawezesha kuimudu vyema fani ya uhandisi.

Makamu Rais wa AngloGold Ashanti - GGML anayeshughulikia miradi endelevu Ghana na Tanzania, Simon Shayo, alibainisha mkakati huo juzi alipozungumza katika Kongamano la Nane la Wahandisi Wanawake (TAWECE) lililofanyika Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar.

Alisema GGML inatambua na kuthamini umuhimu wa wanawake katika fani ya uhandisi hasa kwa kuzingatia ni wabunifu wa kipekee pindi wanapokabidhiwa jukumu, ndiyo maana haikusita kudhamini kongamano hilo lililoshirikisha wanawake wahandisi zaidi ya 800.

Alisema GGML imejikita katika utofauti, usawa na ujumuishaji (DE & I), ambayo ndiyo kiini cha mkakati wa kampuni hiyo katika usimamizi wa wafanyakazi wake.

"Tunaamini kuwapo wahandisi wanawake kunaongeza uwezo wa kampuni yetu na tumeendelea kuweka mazingira ya kuheshimu tofauti na kutoa rukhsa kwa wafanyakazi wote kufikia uwezo wao bila kujali jinsia wala historia yao," alisema Shayo.

Akifungua kongamano hilo, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema Serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Mapinduzi ya Zanzibar, zinatambua na kuthamini mchango wa wahandisi wanawake nchini kutokana na kazi za uhandisi wanazozifanya.

Alisema makongamano kama hayo yamekuwa na mchango mkubwa wa kuunga mkono juhudi za serikali za kuendeleza ubunifu wa sanyansi na kuleta chachu ya maendeleo ya Taifa ikiwamo ujenzi wa viwanda.

Alisema fani ya uhandisi ina umuhimu mkubwa kwa ustawi wa nchi, pia ni uti wa mgongo wa shughuli nyingi za kiuchumi. Hivyo, aliwataka vijana na wanawake kuzitumia fursa zilizopo kuyafikia malengo yao.

Pia aliwashauri wahandisi wanawake kufungua kampuni na kujiajiri kupitia ukandarasi na uhandisi na kueleza hatua hiyo itachangia maendeleo ya nchi kwa kujenga miundombinu imara itakayodumu kwa muda uliokusudiwa.

Rais wa Taasisi ya Wahandisi Tanzania (IET), Gemma Modu alisema takwimu zinaonyesha ushiriki wa wanawake katika uhandisi bado ni mdogo kulinganishwa na wanaume.

Alitaka jamii kuachana na mitazamo potofu juu ya wahandisi wanawake kwa kuangalia upungufu wao unaotokana maumbile ya jinsia zao zikiwamo uzazi na uhalisia wao, na kuwataka waajiri kuona umuhimu wao na kutambua mchango wao kwa maendeleo ya taifa kwa kuwatumia katika kazi za vitendo badala ya kuwapa kazi za ofisini pekee.

Uzinduzi wa kongamano hilo kwa mwaka huu, 2023 ulikwenda sambamba kaulimbiu ya 'Nguvu ya Ushirikishwaji na Uhusishwaji wa Wanawake Katika Kazi za Kihandisi.'

# STAMICO yatangazwa kampuni bora madini Afrika mwaka 2023

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Madini la Taifa (STAMICO) limenyakua tuzo ya Kampuni Bora ya Mwaka Afrika kwenye sekta ya madini 2023 katika Tuzo za Africa Company of the Year Award (ACOYA).

Tuzo hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki katika hafla iliyofanyika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wageni mbalimbali.

Mchakato wa kutafuta washindi umefanywa na kampuni ya Eastern Star Consulting Group Afrika ya Kenya.

Akipokea tuzo hiyo kwa niaba ya shirika, Mkurugenzi Mtendaji, Dk. Venance Mwasse aliyeambatana na Menejimenti ya STAMICO, alisema tuzo hiyo imedhihirisha juhudi za shirika hilo katika kuinua sekta ya madini nchini.

Alisema hatua ya STAMICO kuwa kampuni bora kwa mwaka 2023 imekuwa chachu kwa shirika hilo kuongeza kasi ya utendaji ili kuwanufaisha Watanzania.

"Zaidi ya nchi 15 kutoka Bara la Afrika zilishiriki katika kuwania tuzo hizi na STAMICO iliibuka kidedea kama Kampuni Bora ya Madini Afrika," alisema.

STAMICO imekuwa mfano wa kuigwa Afrika kiasi cha kuivutia Wizara ya Madini na Uchumi wa Bluu ya Kenya ambayo hivi karibuni viongozi waandamizi wa wizara hiyo walikuja nchini kujifunza namna shirika hilo linavyoendeleza shughuli za mnyororo wa thamani wa uchimbaji madini.

Walijifunza namna STAMICO imefanikiwa katika kuendesha shughuli za madini zikiwamo utafiti, uchimbaji, uchakataji na biashara ya madini

Akizungumza katika hafla ya utoaji tuzo hizo, Mkurugenzi wa Africa Company of The Year Awards (ACOYA), Deogratius Kilawe, alisema tuzo hizo zimetolewa nchini mara ya kwanza. Kilawe alizipongeza na kuzishukuru kampuni zote zilizoshiriki na kushinda, akisema lengo la tuzo hizo ni kuongeza ufanisi kwa kampuni katika utoaji huduma kwa wateja wao na wafanyakazi ili kuongeza uwajibikaji kazini.

Mbali na STAMICO kupata tuzo katika hafla hiyo, kampuni zingine zilizopata tuzo ni pamoja na Kampuni ya Ndege ya Uganda (Uganda Airlines), Kampuni ya Kenya Wee Centre - mshindi wa kwanza kwa utunzaji wa mazingira na Kampuni ya Sintel Security ya Kenya iliyoibuka mshindi kwa uchapishaji nyaraka mbalimbali (printing solutions).

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

## TANGAZO LA MWALIKO WA WATAZAMAJI WA UCHAGUZI WA NDANI KATIKA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA MBARALI NA MADIWANI KATIKA KATA SITA ZA TANZANIA BARA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uchaguzi mdogo wa **Ubunge katika Jimbo la Mbarali,** Mkoa wa Mbeya na Madiwani katika kata sita za Tanzania Bara. Uchaguzi huo utafanyika siku ya Jumanne tarehe 19 Septemba, 2023 katika Jimbo tajwa na kata sita ambazo ni: -

| Na. | Kata | Halmashauri |
|---|---|---|
| 1. | Nala | Jiji la Dodoma |
| 2. | Mfaranyaki | Manispaa ya Songea |
| 3. | Mtyangimbole | Wilaya ya Madaba |
| 4. | Mwaniko | Wilaya ya Misungwi |
| 5. | Old Moshi Magharibi | Wilaya ya Moshi |
| 6. | Marangu Kitowo | Wilaya ya Rombo |

Kwa mujibu wa kanuni ya 18 (3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 16(3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za (Uchaguzi wa Madiwani) mwaka 2020, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa mwaliko kwa watazamaji wa uchaguzi wenye nia ya kutazama uchaguzi.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inakaribisha maombi kutoka kwa taasisi na asasi nchini zenye nia ya kutazama uchaguzi mdogo wa **Ubunge Jimbo la Mbarali** na kata sita zilizopo katika halmashauri sita za Tanzania Bara kama ilivyoainishwa kwenye jedwali.

Taasisi na asasi zenye nia ya kutazama uchaguzi huo ziwasilishe maombi kwa kutumia anuani (link) ifuatayo **https://oms.nec.go.tz**
Barua ya maombi pamoja na mambo mengine itatakiwa kuainisha mambo yafuatayo: -

i. Anuani kamili ya taasisi au asasi husika;
ii. Mahali ambapo taasisi au asasi husika inafanyia kazi (Physical address);
iii. Shughuli ambazo zinafanywa na taasisi au asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili;
iv. Maeneo ambayo taasisi au asasi inapenda kwenda kutazama uchaguzi;
v. Idadi ya watu ambao taasisi au asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na majina na taarifa zao binafsi;
vi. Majina na namba za simu za viongozi wa taasisi au asasi husika kama yalivyoandikwa katika hati za usajili;
vii. Ikiwa taasisi au asasi inahusisha watendaji wa kimataifa, viongozi wawili ambao taarifa zao zitawasilishwa ni lazima wawe watanzania;
viii. Kuambatisha nakala au kivuli cha hati ya usajili wa taasisi au asasi husika; na
ix Kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika.

**Maombi yatapokelewa kuanzia tarehe 5 hadi 12 Agosti, 2023.**

**Limetolewa leo tarehe 5 Agosti, 2023 na:**

Kailima, R. K
MKURUGENZI WA UCHAGUZI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

## TANGAZO LA MWALIKO KWA TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA ZENYE NIA YA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA KATIKA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE WA JIMBO LA MBARALI NA MADIWANI KATIKA KATA SITA ZA TANZANIA BARA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha uchaguzi mdogo wa **Ubunge katika Jimbo la Mbarali** na Madiwani katika kata sita za Tanzania Bara. Uchaguzi huo utafanyika siku ya Jumanne tarehe 19 Septemba, 2023 katika Jimbo la Mbarali na kata sita ambazo ni: -

| Na. | Kata | Halmashauri |
|---|---|---|
| 1. | Nala | Jiji la Dodoma |
| 2. | Mfaranyaki | Manispaa ya Songea |
| 3. | Old Moshi Magharibi | Wilaya ya Moshi |
| 4. | Marangu Kitowo | Wilaya ya Rombo |
| 5. | Mtyangimbole | Wilaya ya Madaba |
| 6. | Mwaniko | Wilaya ya Misungwi |

Kwa mujibu wa kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 na kanuni ya 3 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, Tume ina wajibu wa kutoa elimu ya mpiga kura nchi nzima, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inakaribisha maombi kutoka taasisi na asasi za kiraia nchini zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura katika uchaguzi mdogo wa Ubunge Jimbo la Mbarali na kata sita za Tanzania Bara kama ilivyoainishwa kwenye jedwali.

Taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura zinatakiwa kuwasilisha maombi yao kwa njia ya barua pepe: **info@nec.go.tz** au **uchaguzi@nec.go.tz** Maombi hayo yatapokelewa kuanzia tarehe 5 hadi 12 Agosti, 2023.

Barua ya maombi inatakiwa kuainisha mambo yafuatayo kuhusu taasisi na asasi husika:-

i. Iwe imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;
ii. Iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;
iii. Ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu, wawili ambao taarifa zao zitawasilishwa wanapaswa wawe Watanzania;
iv. Katika utendaji wake, iwe haijahusishwa na uchochezi au kuvuruga amani;
v. Iwe na uzoefu wa kutoa elimu ya mpiga kura; na
vi. Iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

Aidha, maombi hayo yanatakiwa kuambatishwa na: -

i. Nakala au kivuli cha cheti cha usajili;
ii. Nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi ya kiraia;
iii. Majina matatu ya viongozi wa juu wa taasisi au asasi ya kiraia;
iv. Anuani kamili ya makazi na namba za simu za ofisi na za viongozi wake; na
v. Ratiba itakayoonesha tarehe na mahali elimu ya mpiga kura itakapotolewa katika halmashauri husika.

Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa taasisi na asasi za kiraia zitakazopewa kibali.

**Limetolewa leo tarehe 5 Agosti, 2023 na:**

Kailima, R. K
MKURUGENZI WA UCHAGUZI



# Zaidi wakulima 100,000 wanufaika mbolea ya ruzuku

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKULIMA 100,559 wa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara, wamenufaika na tani 41,000 za mbolea ya ruzuku zilizotolewa na serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 kwa kuwa itawasaidia kuzalisha mazao yenye tija.

Akifungua maonesho ya Nanenane kwa Kanda ya Kaskazini yenye kaulimbiu: 'Vijana na wanawake ni msingi imara ya mifumo endelevu ya chakula', Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Maulid, alisema serikali imewekeza nguvu kubwa katika kilimo na mifugo kwa lengo la kuinua uchumi wa wakulima, wafugaji na taifa.

"Kati ya mbolea hizo, Mkoa wa Arusha umepata tani 17,288 na kunufaisha wakulima 19,663, Mkoa wa Kilimanjaro tani 19,663 na kuwafikia walengwa 18,067 na Manyara umepatiwa tani 4,840 ambazo zilinufaisha wananchi 62,829," alisema.

Akizungumzia suala la mashamba darasa, alisema kila mkoa kwenye kanda hiyo, ulipata mashamba matatu, huku maofisa ugani wa mikoa hiyo walipewa jumla ya pikipiki 245.

"Pikipiki hizi zimetolewa kuwasaidia maofisa ugani kufikia wakulima na wafugaji kwa urahisi zaidi na hili limeleta matokeo chanya kwa wengi wao kulima kwa kutumia teknolojia za kisasa na kufuga mifugo yenye tija," alisema.

Pia alisema serikali imehakikisha kanda hiyo, kumejengwa kiwanda cha kusindika bidhaa za maziwa na kimekuwa mkombozi mkubwa kwa wafugaji.

Aliwasihi wakulima na wafugaji kujenga utamaduni wa kutumia vituo vya mifugo na uvuvi vinavyomilikiwa na serikali vya uhamilishaji ili kuzalisha mifugo yenye tija.

Kadhalika, aliagiza halmashauri za kanda hizo, kutoa elimu ya ufugaji na kilimo bora kwa kutoa asilimia 10 ya mikopo inayotolewa kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu iwasaidie kuimarisha uchumi kupitia mifugo na kilimo.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alimshukuru Spika na timu ya Wawakilishi kutoka Zanzibar, ambao wameshiriki maonesho hayo kwa mara ya kwanza na kupata wageni kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ).

Alisema zaidi ya asilimia 60 ya wananchi wa mikoa hiyo, hujikita kwenye sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi na kwamba ni muhimu kwa ukuzaji wa uchumi na upatikanaji wa mnyororo wa thamani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Nanenane, ambaye ni Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Missaile Mussa, alisema maonesho yameshirikisha washiriki zaidi 800 zikiwamo kampuni za mbegu, zana za kilimo, usindikaji wa mazao ya kilimo, uvuvi na mazingira, elimu na watoa huduma.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alisema maonesho yalianza mwaka 2016 yakiratibiwa vyema na Makatibu Tawala wa mikoa husika, yameratibiwa vizuri na ameishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa kuinua kilimo kuwa cha kisasa kwa kutumia teknolojia za kisasa.

"Tunapozungumzia mafanikio haya katika sekta ya kilimo na mifugo, lazima tumpongeze Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kunufaisha kanda yetu, kupitia Filamu ya The Royal Tour iliyoongeza watalii na mapato kwa kuwa imetusaidia kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 143, mwaka huu wa fedha, kutoka Sh. bilioni 73 kwa mwaka 2022 kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini," alisema.



Ofisa Tarafa ya Kwekivu, Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga, Michael John (wa tatu kulia), akishirikiana na wakazi wa Kijiji cha Kwedibo kuchimba udongo kwa ajili ya kufyatua tofali za ujenzi wa madarasa ya Shule ya Msingi Kwedibokwa alipofanya ziara shuleni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Waomba askari wa kike kupelekwa Kituo cha Polisi Komolo

**Na Allan Isack, SIMANJIRO**

WAKAZI wa Tarafa ya Terrat wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wameiomba serikali kuwapeleka askari polisi wa kike kwenye Kituo cha Polisi cha Komolo kwa kuwa wanawake wanakamatwa na askari wa kiume kitendo ambacho ni kinyume na utaratibu wa Jeshi la Polisi.

Hayo yamebainika kwenye kongamano la mradi wa Tanzanite Uchumi Imara wa Mwanamke, katika Mji Mdogo wa Mirerani wilayani humo, lililoandaliwa na shirika lisilo la kiserikali la Civil Social Protection Foundation (CSP).

Mmoja wa wakazi wa Kata ya Terrat, Scola Lukumay, amemwomba Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera, kuwasaidia ili waweze kupata askari wa kike.

"Kwenye kituo cha polisi Komolo, hakuna askari polisi wa kike hivyo wanawake wanakamatwa na askari wa kiume na kitendo hicho ni ukiukaji wa haki za binadamu tunaomba askari wa kike," alisema.

Alisema ni vyema serikali ikaangalia usawa wa kijinsia wa askari wa kike, kwa kuwa kwa sasa wananchi wa eneo hilo na tarafa hiyo wanakwazika.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera, alisema amepokea ombi hilo na atahakikisha jitihada za dhati zinafanyika ili askari wa kike wapatikane katika kituo hicho.

"Hilo nimelichukua nitazungumza na OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya), ambaye bado ni mgeni ili aweze kupanga askari wa kike kwenye kituo hicho cha polisi Komolo," alisema Dk. Serera.

Mwanasheria wa CSP, Eliakim Paulo, amesema lengo la kongamano hilo ni kuangalia matatizo na kero zinazowakabili wanawake wanaozunguka machimbo ya madini ya Tanzanite.

"Tumeona tufuatilie ahadi zilizotolewa hivi karibuni tulipokutana na baadhi ya viongozi wa serikali kama zimetimizwa katika sekta mbalimbali," alisema Paulo.

Kongamano hilo, limebaini kuwa asilimia kubwa ya matatizo yaliyokuwa yanalalamikiwa na wanawake wa eneo hilo yamefanyiwa kazi.

# Viongozi watakiwa kutoa maelekezo kwa maandishi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Seif Shekalaghe, ameagiza watumishi wa wizara hiyo, wanapopewa maelekezo ya mdomo kutoka kwa viongozi wao wahakikishe kuwa wanaandika barua ambayo itasainiwa na kiongozi husika ili kuwapo kwa kumbumbuku ya uthibitisho.

Agizo hilo limetolewa jana jijini Arusha na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dk. Japhet Simeo, kwa niaba ya Dk. Shekalaghe, akifunga mafunzo ya siku 11 ya menejimenti, uongozi na utawala kwa wataalamu 43 wa afya kutoka halmashauri 11 za Mkoa wa Tanga yaliyofanyika kwenye Taasisi ya Elimu ya Watumishi wa Afya Arusha (CEDHA).

Alisema baadhi ya watumishi wamejikuta wakiingia kwenye kasumba ya kupokea maelekezo kutoka kwa viongozi wao bila ushahidi wa kuthibitisha kwa maandishi jambo waliloagizwa.

"Mnapopewa maelekezo ya mdomo na viongozi wenu, hakikisheni mnaandika barua ya kukubali maelekezo hayo na asaini ili kuwapo kwa kumbukumbu kwenye jalada endapo ikatokea siku moja kuna tatizo na umeitwa popote utakuwa na ushahidi wa kujitetea," alisema.

Aliwataka watumishi wa sekta hiyo (viongozi), ngazi za wilaya na mkoa kujenga uaminifu na moyo wa kusamehe na kuwatetea hadharani wenzao wanapokosea, lakini wanapokwenda kwenye vikao vyao vya ndani waambiane ukweli.

"Usitafute makosa kumkomoa au kumuumiza mtu badala yake tafuta ushahidi wa kumsaidia kwa kuwa uongozi siyo njia ya kujitetea pale makosa yanapotokea na kwenye taasisi yetu sisi kama viongozi tujitahidi kusoma hulka na silka za watu tunaowaongoza," alisema.

Naye Naibu Meneja wa Programu ya Uboreshaji wa Huduma za Afya hapa nchini, kutoka Shirika la Kimataifa la Maendeleo la nchini Ujerumani (GIZ), Erick Msoffe, alisema mafunzo hayo yamewezeshwa na shirika hilo kwa kwa kushirikiana na CEDHA kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalamu hao.


Aidha alisema kutoka na kuwapo kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Ujerumani kwa zaidi ya miaka 20 hasa kwenye sekta ya afya wamefanya kazi kubwa katika mikoa mbalimba hapa nchini.

Vile vile, alisema wamefikia hatua ya kuwesha mafunzo hayo,kwa kuwa shirika hilo limejikita kwenye mambo makuu matatu ikiwamo suala la watu, sera na mchakato.

"Kutokana na mambo haya matatu tumeweza kuwa na sera bora ambazo zimejikita zaidi kutoa huduma kwa watu kwa kuwa ndiyo msingi halisi," alisema Naibu Meneja huyo wa GIZ.

Mkuu wa CEDHA, Dk. Johaness Lukumay, alisema taasisi hiyo ya serikari, imepewa majukumu ya kuendeleza watumishi wa afya katika kada mbalimbali.

Pia Dk. Lukumay, taasisi hiyo, ina jukumu la kuwafundisha wakufunzi wa taaluma za afya ili kuhakikisha wanatoa mafunzo stahiki kwa walengwa, kufanya utafiti wa kutatua changamoto za afya na kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu.





# Kamishna Shilogile asisitiza amani Tarime

**Na Timothy Itembe,** MARA

KAMISHNA wa Kamisheni ya Polisi Jamii CP Faustine Shilogile, amewataka viongozi mbalimbali wakiwamo wa dini wilayani Tarime kudumisha na kuhubiri amani na utulivu katika jamii kusaidia kukomesha vitendo vya kihalifu.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akiongea na viongozi mbalimbali wa serikali, madhehebu ya dini taasisi zisizokuwa za serikali na vyama vya siasa kuhusu utekelezaji wa mwongozo wa kufichua na kuzuia uhalifu nchini.

"Lengo ni kuzuia uhalifu kwa njia shirikishi kila mdau atambue wajibu na nafasi yake katika suala la kushirikiana kudhibiti vitendo vya uhalifu ndani ya jamii," alisema CP Shilogile.

Katika vikao hivyo wananchi wa Kijiji cha Weigita, waliibua hofu kuhusu hali ya usalama inayowanyemelea baina yao na Kijiji cha Matongo kuwapo mgogoro wa muda mrefu wa mpaka wa kiutawala ambao tayari umewasilishwa katika uongozi ngazi za wilaya, lakini haujatatuliwa na kuomba kufikisha sehemu husika.

Kuhusu suala hilo, Shilogile alisema atalifikisha kwa viongozi ngazi ya juu na kuwataka viongozi wa vijiji, madiwani na Mkuu wa wilaya kulishughulikia kijamii ili kurejesha amani na kuondoa wasiwasi uliopo ya kuashiria uvunjifu wa amani.

Ofisa Polisi wa Dawati la Jinsia makao makuu, Faida Suleman, aliwataka wananchi kuwa na utaratibu wa kuhudhuria dawati la polisi ili kupata ushauri kuhusu matatizo na migogoro mbalimbali ikiwamo ya kifamilia.

Alisema kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ameruhusu na kuboresha madawati ya polisi ikiwamo viongozi wake kupata mafunzo ili kutumikia wananchi kwa ufanisi.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, akigawa uji wa lishe kwa watoto na kuwahimiza wazazi mkoani humo wawapatie watoto lishe bora pamoja na kuwanyonyesha maziwa ya mama ili wakue kimwili na kiakili, amegawa uji huo juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Lishe na Wiki ya Unyonyeshaji mkoani humo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Kinamama wakumbushwa umuhimu kunyonyesha watoto

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amekumbusha kinamama mkoani humo kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya kuhusu unyonyeshaji watoto maziwa ya mama pamoja na lishe bora lengo likiwa ni kuwa na watoto wenye afya njema kimwili na kiakili.

Alitoa kauli hiyo juzi kwenye maadhimisho ya siku ya lishe na wiki ya unyonyeshaji Mkoa wa Shinyanga yaliyofanyika na kueleza kuwa maziwa ya mama kwa mtoto yana virutubisho pamoja na kinga ya mwili na kuwataka kutowanyima watoto haki yao.

"Mtoto akizaliwa baada ya saa moja, anapaswa kunyonyeshwa na anyonyeshwe yale maziwa ya kwanza ya njano na siyo kuyakamua na kuyamwaga yanavirutubisho tosha kabisa na hayana madhara," alisema Mndeme.

"Mtoto pia anapaswa kunyonyeshwa ndani ya miezi sita bila kupewa chakula chochote wala maji na wakati ukifika wa kumpatia vyakula vya ziada lizingatiwe suala la lishe bora huku akiendelea kunyonyeshwa hadi afikishe miaka miwili," aliongeza.

Aliwataka waajiri wa sekta binafsi kutoa fursa kwa wafanyakazi waliojifungua kupata muda wa kunyonyesha na kutengewa chumba maalumu kwa ajili ya kumhudumia mtoto ili watoto wapate haki ya maziwa ya mama bila kujali kazi ya mzazi.

Ofisa lishe Mkoa wa Shinyanga, Yusuph Hamisi, alisema ni asilimia 30 pekee kinamama katika Mkoa wa Shinyanga ambao wananyonyesha watoto wao ndani ya saa moja baada ya kujifungua na kuwasisitiza kuwa maziwa ya mama kwa mtoto ni muhimu sana katika afya yake na ukuaji kimwili na kiakili.

Aliwasisitiza pia kinamama wazingatie suala la lishe bora kwa watoto wao kwa kuzingatia makundi matano ya vyakula. Nao baadhi ya kinamama akiwamo, Kareny Jamsoni, walitoa ushuhuda kwa wanawake wenzao, namna walivyozingatia suala ya unyonyeshaji kwa mtoto wake ndani ya miezi sita bila ya kumpatia kitu chochote kile cha kula na sasa ana afya njema.

# Vijiji vinne vyamtunuku beberu Rais Samia

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAIDI ya wakazi 15,000 kutoka vijijini vinne vya Kata ya Nyamilangano, Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, vimemtunuku zawadi ya mbuzi beberu Rais Samia Suluhu Hassan baada yakutekeleza ahadi yake ya kujengwa kwa Hopsitali ya Wilaya ya Ushetu na kuanza kutoa huduma.

Wakazi wa vijiji hivyo vya Nyamilango, Ididi, Hundi na Mitonga awali walilazimika kutembea umbali wa kilometa 50 kwenda Hospitali ya Manispaa ya Kahama kupata matibabu huku baadhi yao wakiwamo wajawazito walilazimika kujifungulia njiani na nyumbani.

Akikabidhi beberu hilo kwa kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa, Abdallah Kaim kwa niaba ya Rais Samia hivi karibuni, Diwani wa Nyamilangano, Robert Mihayo, alisema hiyo ni zawadi ya Rais kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi yake katika miradi ya maendeleo hususan katika sekta ya afya, elimu, maji na miundombinu ya barabara.

Alisema, wananchi wametoa zawadi ya mbuzi wawili, mmoja wa Rais Samia kwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati na kuanza kutoa huduma kwa wananchi huku mwingine akiwa ni wa kiongozi huyo wa mbio za Mwenge.

Mkazi wa Kijiji cha Mitonga, Sakina Juma, alisema kabla ya kuwapo kwa hospitali ya wilaya walilazimika kusafiri kwenda vituo vya afya Bulunga, Iboja na Ushetu-Mbika na walipokosa baadhi ya huduma walilazimika kusafiri hadi Hospitali ya Manispaa ya Kahama kwa gharama kubwa.

"Tumetoa mbuzi huyo kwa moyo mkunjufu kabisa kwani gharama zake hazifikii hata zile tulizokuwa tukizitoa katika kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma za afya hususani kwetu wanawake wajawazito," alieleza Sakina.

Kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa, Abdallah Kaim, aliahidi kufikisha zawadi hiyo kwa Rais Dk. Samia Suluh Hassan na kuwataka kuitunza miradi hiyo ili izidi kuwanufaisha.

Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani alisema, wananchi wa Ushetu wana uhitaji mkubwa wa maji kwa kuwa mpaka sasa usanifu umefanyika wa kupata mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria na utakavyoanza utekelezaji wananchi wachangamke fursa za ajira za muda na kujiongezea kipato cha kaya.

Nipashe
Spotika




'BIG SIX' ZA EPL ZILIZOFANYA USAJILI BORA MSIMU 2023-24 UK. 12-13




DE BRUYNE

# WACHEZAJI WA5 WENYE MAONO BORA ZAIDI DUNIANI

## ISIKUPITE

WACHEZAJI watano bora ambao wameondoka 'Premier League' Ligi Kuu England katika dirisha hili la usajili la majira ya joto, #1 Riyad Mahrez (Manchester City kwenda Al-Ahli), #2 N'Golo Kante (Chelsea kwenda Al-Ittihad), #3 Roberto Firmino (Liverpool kwenda Al-Ahli), #4 Jordan Henderson (Liverpool kwenda Al Ettifaq) na #5 Allan Saint-Maximin (Newcastle United kwenda Al-Ahli).




**LONDON,** England

KATIKA soka, uwezo wa mchezaji kutambua na kuchambua mchezo unaoendelea karibu naye huelezewa kuwa maono. Inazungumzia uelewa wa mchezaji uwanjani, wana kuwa na uwezo kutambua mienendo ya wachezaji wenzake na wapinzani na kufanya maamuzi ya haraka.

Wachezaji soka wenye maono makubwa wanaweza kuona nafasi, mapungufu na fursa katika safu ya ulinzi ya wapinzani. Pia wataweza kupiga pasi sahihi, iwe fupi au mipira mirefu na kutengeneza nafasi kwa wenzao.

Mchezaji anasemekana kuwa na maono mazuri wakati chaguzi zao za kimkakati ni bora mara kwa mara kuliko zile za wengine.

Wachezaji kama Andres Iniesta, Xavi na Paul Scholes ni mifano mizuri ya wachezaji wenye maono mazuri. Sasa, tuwatazame wachezaji watano wenye maono bora zaidi katika soka la dunia hivi sasa...

### #5 Martin Odegaard (Arsenal)

Martin Odegaard sasa amejidhihirisha kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi barani Ulaya. Nahodha huyo wa Arsenal alikuwa na mchango mkubwa katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu England kwa 'Washika Bunduki' hao msimu uliopita licha ya kutoweza kubeba, akielekeza kwa ustadi masharti ya kiungo na sifa za kipekee.

Ustadi wa kiuchezaji wa kiungo huyo wa Norway unaimarishwa na maono yake, ambayo yanamruhusu kupenyeza pasi sahihi kupitia nafasi zilizobana na hivyo kufungua ulinzi. Uwezo wake wa kuona nafasi za wazi, mienendo ya wachezaji wenzake na kutoa pasi za kiubunifu humfanya awe na nguvu ya kuzingatiwa haswa katika katika tatu ya mwisho.

Alifunga mabao 15 na kutoa asisti nane katika mechi 45 kwenye mashindano yote akiwa na Arsenal msimu uliopita.

### #4 Antoine Griezmann (Atletico Madrid)

Antoine Griezmann ni mmoja wa washambuliaji bora wa kizazi chake na uwezo wake wa soka unakuzwa na maono yake. Yeye ni mwenye nguvu uwanjani kutokana na uwezo wake wa ndani wa kuusoma mchezo.

Fowadi huyo wa Atletico Madrid anaweza kutathmini kwa haraka hali mbalimbali zinazotokea mbele yake na kurekebisha uchezaji wake ipasavyo. Maono ya ajabu ya Griezmann yanaakisiwa katika harakati zake na mara nyingi hukimbia bila mpangilio na kutokea katika nafasi zilizo wazi.

Griezmann pia ni mmoja wa wachezaji walio na vipaji vya kiufundi zaidi wa kizazi chake na uwezo wake sahihi wa kupiga pasi umesaidia kumpandisha kwenye safu ya wachezaji mahiri. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, alifunga mabao 16 na kutoa asisti 19 katika mechi 48 kwenye mashindano yote akiwa na 'Rojiblancos' hao msimu wa 2022-23.

### #3 Bruno Fernandes (Manchester United)

Bruno Fernandes ametengeneza nafasi nyingi (254), kwenye Ligi Kuu England tangu ajiunge na Manchester United Januari 2020 kuliko mchezaji mwingine yeyote kwenye mashindano hayo.

Kevin De Bruyne, anayetajwa kuwa kiungo mbunifu zaidi duniani, anashika nafasi ya pili kwenye orodha hiyo akiwa ametengeneza nafasi 235 katika kipindi hicho.

Fernandes amecheza nafasi kubwa kwa 'Mashetani Wekundu' katika misimu ya hivi karibuni na ndiye mchezaji muhimu zaidi katika kikosi chao. Kwa kukosekana kwake, United wanaweza kuonekana wajinga na wasio na la kufanya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alitoa pasi za mabao 15 pamoja na kufunga mabao 14 katika mechi 59 kwenye mashindano yote akiwa na Manchester United msimu uliopita.

### #2 Lionel Messi (Inter Miami)

Lionel Messi ana ufahamu mkubwa wa mchezo na bila shaka yoyote ndiye mwanasoka bora zaidi wa wakati wote. Mbali na kuwa mmoja wa wafungaji bora katika historia ya mchezo huo, Messi pia amesimama kwa maono yake ya ajabu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, ana uwezo wa kutafuta njia za kupita na kutengeneza nafasi ambazo haziwezi kufikiwa na wenzake wengi. Gwiji huyo wa Argentina amepoteza kasi katika miaka ya hivi karibuni. Lakini anaendelea kuwa mmoja wa wachezaji bora katika mchezo huo kutokana na ujuzi wake wa ajabu wa kucheza na maono.

Messi alifunga mabao 21 na kutoa asisti 20 katika mechi 41 kwenye mashindano yote akiwa na PSG msimu wa 2022-23.

### #1 Kevin De Bruyne (Manchester City)

Kukusanya pasi 31 za mabao kwenye mashindano yote katika msimu wa kihistoria wa kushinda mataji matatu kunapaswa kuwa uthibitisho wa kutosha wa maono ya ajabu ya mchezaji na ustadi wa kucheza. De Bruyne ndiye kiungo bora zaidi wa kizazi chake.

Nyota huyo wa Ubelgiji ameonesha maono yake ya ajabu uwanjani, akiona fursa ambazo wachezaji wengine wanaweza kukosa. Mara nyingi anaonekana akitengeneza nafasi za kufunga bila kitu na ana uelewa usio na kifani wa mchezo.

De Bruyne ni mwenye maono na ataingia katika historia ya kuwa mmoja wa wachezaji bora wa zama za Ligi Kuu England.



ANDRE ONANA

# 'BIG SIX' ZA EPL ZILIZOFANYA USAJILI BORA MSIMU 2023-24

**LONDON,** England

MSIMU wa Ligi Kuu England wa 2023-24 unaoanza Ijumaa hii kwa maana zimebakiza siku tatu tu kabla ya kuanza. Mabingwa Watetezi wa ligi hiyo, Manchester City, watacheza na Burnley iliyopanda daraja, Agosti 11, mwaka huu ili kuanza kampeni mpya.

**Kwa wiki kadhaa zilizopita, klabu zimekuwa zikijiandaa kwa ajili ya msimu mpya kwa kushiriki katika mechi za kirafiki za kabla ya msimu mpya na pia zikifanya makubwa kwenye soko la uhamisho wa wachezaji majira haya ya joto.**

Dirisha la usajili ni wakati muhimu kwa klabu sita kubwa 'Big Six' kwani ubora wa mikataba wanayofanya katika kipindi hiki inaweza kuwa na mchango mkubwa kwenye mafanikio yao msimu huu. Zaidi ya hayo, kuambatana na wapinzani wengine kati ya sita bora kunamaanisha kila klabu lazima iandae kikosi chenye uwezo kwa ajili ya msimu.

Kwa klabu za Ligi Kuu England, dirisha la uhamisho wa wachezaji halijafungwa hadi Septemba Mosi, mwaka huu. Hata hivyo, wakati msimu mpya ukiwadia, makala haya yanaangalia kwa kina jinsi klabu hizo za 'Big Six' zilivyofanya hadi sasa kwenye soko la uhamishaji linaloendelea.

Bila kuchelewa zaidi, tunazitazama klabu sita kubwa za Ligi Kuu England kulingana na aina ya wachezaji waliosajili hadi sasa...

### #6 Manchester City

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England, Manchester City ndio imekuwa klabu iliyosajili wachezaji wachache kati ya klabu kubwa sita bora msimu huu wa majira ya joto hadi sasa. Hakuna jambo la kushangaza kwani Pep Guardiola bado ana kiini cha kikosi chake kilichoshinda mataji matatu msimu uliopita.

Hadi sasa Man City wamekamilisha dili moja pekee. Mateo Kovacic alijiunga na mabingwa hao mara sita wa Ligi Kuu kutoka Chelsea kwa kitita cha pauni milioni 25, akichukua nafasi ya Ikay Gudogan aliyehamia Barcelona kwa uhamisho wa huru.

Hata hivyo, City imekuwa ikihusishwa na kutaka kumsajili Josko Gvardiol na wanapewa nafasi kubwa ya kumnasa beki huyo wa Croatia. Kwa mujibu wa mwandishi wa habari za usajili, Fabrizio Romano, klabu hiyo imefikia makubaliano binafsi na mchezaji huyo, lakini bado haijakamilisha makubaliano na RB Leipzig.

Pia kuna uwezekano mkubwa kwamba City wanaweza kufanya usajili wa ziada kabla ya dirisha kufungwa. Riyad Mahrez alijiunga na Al-Ahli hivi majuzi, na kuna uwezekano kwamba klabu hiyo inaweza kuwa inatafuta mchezaji mpya wa kuziba pengo la Mualgeria huyo.

### #5 Tottenham Hotspur

Tottenham imefanya kazi kubwa msimu huu wa majira ya joto. Wamemleta kocha mpya na kuongeza majina mapya kwenye orodha ya kikosi chao. Kocha wa zamani wa Celtic, Ange Postecoglou ataiongoza klabu hiyo katika msimu mpya.

Spurs wamemsajili kiungo wa kati wa England, James Maddison kutoka Leicester City iliyoshuka daraja kwa pauni milioni 40. Pia wamemsajili Guglielmo Vicario kutoka Empoli kwa pauni milioni 17.

Mshambuliaji huyo wa Italia atachukua nafasi ya Hugo Lloris ambaye anasaka klabu mpya baada ya kuachwa kwenye kikosi cha maandalizi ya msimu mpya.

Mshambuliaji wa Israel, Manor Solomon pia alijiunga na klabu hiyo ya Kaskazini mwa London kwa uhamisho wa huru kutoka Shakhtar Donetsk. Mikataba ya mkopo ya Pedro Porro na Dejan Kulusevski imefanywa kuwa ya kudumu pia.

### #4 Chelsea

Chelsea imekuwa klabu yenye shughuli nyingi zaidi kati ya timu kubwa sita katika masuala ya uhamisho wa jumla katika dirisha la sasa. Marekebisho makubwa katika Uwanja wa Stamford Bridge yamewafanya wachezaji 10 wa kikosi cha kwanza kuondoka msimu huu.

Mason Mount, Mateo Kovacic na Kai Havertz wamejiunga na wapinzani wao wa Ligi Kuu Manchester United, Manchester City na Arsenal. Edouard Mendy na Kalidou Koulibaly, wamehamia Saudi Arabia huku N'Golo Kante na Cesar Azpilicutea pia wakiondoka kwa uhamisho huru. Wachezaji wengine ambao wameondoka 'Blues' ni pamoja na Pierre Emerick Aubameyang, Christain Pulisic na Ruben Loftus-Cheek.

Kumekuwa na wachezaji wawili wakuu waliowasili katika klabu hiyo hadi sasa. Christopher Nkunku (pauni milioni 52) na Nicolas Jackson (pauni milioni 32) walinaswa kutoka kwa RB Leipzig na Villareal ili kuimarisha safu ya ushambuliaji.

Vijana Angelo Gabriel na Diego Moreira pia wamenaswa na klabu hiyo. Angelo, Mbrazil amejiunga kutoka Santos, wakati Moreira mwenye umri wa miaka 18, ametua kwa uhamisho huru kutoka Benfica.

### #3 Liverpool

Baada ya kampeni mbaya ya 2022-23, ilionekana wazi kuwa Liverpool ilihitaji vipaji vipya katika klabu hiyo. Hasa katika idara ya kiungo ambapo waliteseka sana kutokana na majeraha kwa baadhi ya wachezaji wao muhimu.

Ili kuchukua wachezaji wapya, ilikuwa ni lazima kuwaondoa wale ambao hawakuwa wakicheza kwa viwango. Naby Keita, James Milner, Roberto Firmino, na Alex Oxlade-Chamberlain wote wameondoka kama wachezaji huru.

Kuziba pengo la kiungo, 'Wekundu' hao wametumia pauni milioni 95 kuwanunua Dominik Szoboszlai na Alexis MacAllister kutoka RB Leipzig na Brighton & Hove Albion.

Usajili zaidi unatarajiwa kutoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu wa mwaka 2020 ambao walimpoteza Jordan Henderson hivi karibuni kwa Al-Ettifaq. Fabinho pia amejiunga na Al-Ittihad.

### #2 Manchester United

Manchester United wana wachezaji wawili wakubwa waliosajiliwa hadi sasa. Mason Mount kutoka Chelsea (pauni milioni 60), na Andre Onana kutoka Inter Milan ambaye amechukua nafasi ya David De Gea aliyeondoka. Beki wa zamani Johnny Evans pia alisaini mkataba wa muda mfupi wa kujiandaa na msimu mpya na klabu hiyo.

'Mashetani Wekundu' hao pia wamekubali dili la kumsajili fowadi wa Atlanta, Rasmus Hojlund. Kama ilivyoripotiwa kupitia gazeti la The Mirror, mchezaji huyo wa Kimataifa wa Denmark ataigharimu timu hiyo pauni milioni 72.

### #1 Arsenal

Baada ya kukosa ubingwa wa Ligi Kuu msimu uliopita, ilidhihirika wazi kwamba klabu hiyo ya London inahitaji moto zaidi ili kuweza kuchuana na timu nyingine kubwa, hasa Manchester City.

Arsenal kwa kiasi kikubwa imekuwa ikifanya kazi zaidi katika soko la usajili linaloendelea katika 'Big Six'. Hii ni kwa sababu 'Washikabunduki' hao wametumia fedha nyingi zaidi kwa uhamisho unaoingia hadi sasa.

Kwa mujibu wa soko la uhamisho, timu hiyo ya Mikel Arteta imetumia euro milioni 231.60 kupata wachezaji watatu tu msimu huu wa majira ya joto. Declan Rice alichukuliwa kutoka West Ham United kwa ada ya rekodi ya klabu ya pauni milioni 105. Kai Havertz na Jurrien Timber pia wamejiunga na Washikabunduki hao kutoka Chelsea na Ajax.

## Nukuu

"Niwahakikishie Wanasimba wote, tuna timu imara msimu huu, tuna wachezaji zaidi ya wawili kwenye kila nafasi, naupongeza uongozi wa klabu kwa kufanya usajili huu mkubwa. Simba ni timu kubwa na tuna malengo ya kuchukua ubingwa wa ndani na kufanya vizuri kwenye michuano ya kimataifa," **Kocha Mkuu wa Simba Robertinho Oliveira.**



"Nadhani Declan Rice ni mchezaji mzuri ambaye ataifanya Arsenal kuwa bora zaidi. Anaweza kuja katika timu na kutekeleza majukumu ya wachezaji wawili - anaweza kuwa Xhaka na Partey katika Arsenal moja na hiyo inawaweka huru wachezaji wao wabunifu. Unaweza kuona jinsi nyongeza yake itakavyomfanya [Martin] Odegaard kuwa mchezaji hatari zaidi. Atafungua zaidi uwezo wa Arsenal wa kushambulia. Nadhani ni ununuzi mzuri sana kwa Arsenal," **Mshambulizi wa zamani wa Tottenham Hotspurs, Teddy Sheringham, akitoa maoni yake namna Odegaard atakuwa hatari zaidi baada ya Rice kuwasili Arsenal.**



"Sijui jinsi Luis Suarez anaweza kuondoka Gremio. Lakini kama atafanya hivyo, tuko huru kuzungumza na Luis na kumleta Inter Miami. Uwezekano huo ungekuwa pale. Ninamchukulia kama mchezaji nyota, mwenye taaluma ya ajabu. Na sote tunajua ana uhusiano wa binafsi na Lionel [Messi], Busi [Sergio Busquets] na Jordi [Alba]," **Mmiliki mwenza wa Inter Miami, Jorge Mas.**






Mashabiki wa Simba waliofurika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana kusherehekea Simba Day yao, mmoja akionyesha ni shabiki mkubwa wa Luis Miquissone 'Konde Boy'. **MPIGAPICHA WETU**

# REKODI TANO KALI ZA TAMASHA SIMBA DAY

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba jana ilisherehekea tamasha lake la kila mwaka, 'Simba Day', ilipocheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Power Dynamos ya Zambia.

Waliofurika uwanjani na kuangalia kwenye televisheni walishuhudia kutangazwa benchi la ufundi na wachezaji wote wa kikosi cha msimu wa 2023/24, wakiwamo wachezaji wapya na wanaorejea tena kwenye kikosi hicho.

Baadhi ya hao ni Aubin Akramo aliyesajiliwa kutoka Asec Mimosas ya Ivory Coast, Willy Onana kutoka Rayon Sport ya Rwanda, Che Fondon Malone aliyechukukuliwa kutoka Cotonsport ya Cameroon, pamoja na urejeo wa winga wa zamani wa timu hiyo, Luis Miquissone.

Mbali na hilo kulikuwa na burudani mbalimbali za muziki wa dansi pamoja na wanamuziki mbalimbali wa Singeli, Hip Hop na Bongo Fleva, waliokuwa wakitumbuiza kabla ya mechi yenyewe kuhitimisha tamasha hilo.

Litakuwa ni tamasha la 15 tangu lilipoasisiwa mwaka 2009 na aliyekuwa Mwenyekiti wa Klabu hiyo mwaka huo, Hassan Dalali 'Field Marshal', ambapo wanachama na mashabiki wa klabu hiyo huanza kwa kufanya kazi na shughuli za kijamii, ikiwamo kutoa misaada kwenye vituo vya watoto yatima, hospitalini, magereza.

Shughuli hizo hufanyika kwa matawi mbalimbali ya wanachama nchi nzima, pamoja na kuchangia damu ili kuwasaidia wahitaji.

Makala haya inawaletea rekodi ambazo zimewekwa tangu kuanzishwa kwa tamasha hilo 2009 ilipocheza kwa mara ya kwanza dhidi ya SC Villa ya Uganda na kushinda bao 1-0.

### #1. Hakuna mchezaji wa 2009 lilipoanzishwa

Simba jana ilicheza mechi yake ya 15 ya tamasha lake bila kuwa na mchezaji yeyote aliyekuwamo kwenye kikosi kilichocheza mechi ya kwanza 2009.

Rekodi inaonyesha kuwa mechi hiyo ilichezwa Uwanja wa Taifa Dar es Salaam (sasa Uhuru), Agosti 8, mwaka huo, Simba ikishinda bao 1-0 lililofungwa na Hilary Echessa dakika ya nane ambaye alikuwa amesajiliwa kwa mara ya kwanza kutoka nchini Kenya.

Ikiwa chini ya kocha Mzambia Patrick Phiri, ikiwa na baadhi ya wachezaji kama Emmanuel Okwi na Joseph Owino, ambao nao walikuwa wamesajiliwa kwa mara ya kwanza kutoka Uganda.

### #2. Mkude nje baada ya miaka 12

Aliyekuwa kiungo mkabaji wa timu hiyo, Jonas Mkude alikosekana kwa mara ya kwanza kwenye Simba Day baada ya miaka 12.

Kwa mara ya kwanza Mkude alitambulishwa msimu wa 2011/12 akiwa amepandishwa kutoka kikosi cha pili na muda mrefu amekuwa kwenye kikosi hicho na mpaka msimu uliopita alikuwa ndiye mchezaji aliyekaa miaka mingi Simba na mwenye Simba Day nyingi zaidi kuliko yeyote yule.

Angeendelea na rekodi hiyo kama angebakishwa na klabu yake ili kufikisha miaka 13, lakini alionyeshwa mlango wa kutokea na sasa amesajiliwa na Klabu ya Yanga.

### #3. Tshabalala aongoza Simba Day

Beki wa kushoto wa klabu hiyo, Mohamed Hussein 'Tshabalala' au 'Zimbwe Jr', ndiye aliyecheza mechi nyingi za Simba Day kuliko mchezaji mwingine yeyote kwa sasa katika kikosi hicho.

Jana alitambulishwa mara ya 10 kwenye tamasha hilo, akiwa pia mchezaji wa muda mrefu aliyebaki kwenye kikosi hicho aliyecheza mfululizo.

Mchezaji huyo aliibukia kwenye kikosi cha pili cha Azam FC chini ya miaka 19, mwaka 2013 na akachukuliwa na Kagera Sugar akicheza kwa msimu mmoja wa 2013/14 kabla ya kunyakuliwa na Simba 2014 ambapo tangu hapo si tu amekuwa kwenye kikosi hicho kwa misimu yote mfululizo, bali akiwa tegemeo pia.

### #4. Kapombe mkongwe aliyerejea

Kama si kuihama timu hiyo na kurejea tena 2017, Shomari Kapombe ndiye angekuwa mchezaji pekee aliyecheza Simba Day nyingi zaidi.

Angekuwa amecheza mara 13 na kuweka rekodi hiyo kama asingeondoka kwenda Cannes ya Ufaransa mwaka 2013 na hata aliporejea alijiunga na Azam FC mwaka 2014 hadi 2017 ndipo aliporejea tena klabu ya Simba na kuitumikia hadi leo hii.

Amezikosa Simba Day nne kuanzia 2013 hadi 2016, hivyo amecheza tisa ingawa si kwa mfululizo kama Tshabalala ambaye ana 10 zilizonyooka.

Kapombe alijiunga na Simba mwaka 2011 akitokea Polisi Morogoro na kuanza moja kwa moja kuchezeshwa mechi za Ligi Kuu kutokana na kipaji kikubwa alichokuwa nacho, hasa uwezo wake wa kucheza namba nyingi uwanjani, ingawa alikuwa amesajiliwa kama mchezaji wa kikosi cha pili, kabla ya kupandishwa msimu uliofuata.

### #5. Simba Day ya kwanza kwa Miquissone

Utashangaa kuona kuwa jana ilikuwa ni Simba Day ya kwanza kwa winga Luis Miquissone kwenye kikosi cha Simba kama wachezaji wenzake waliosajiliwa msimu huu.

Pamoja na kwamba aliwahi kuichezea msimu wa 2021/22, lakini wakati wa tamasha hilo aliomba ruhusa kwenda kwao Msumbiji kuoa, msimu uliofuata hakuweza tena kutambulishwa kwa sababu aliuzwa Klabu ya Al Ahly ya Misri.

Mchezaji huyo alithibitisha hilo mwenyewe kabla ya mechi ya jana.

"Nimerudi kwa sababu ya mashabiki wangu, mara ya kwanza nipokuwa na timu hii sikuwapo kwenye Simba Day, nilikwenda kuoa, mara ya pili nilikuwa nimeshaondoka kwa hiyo natarajia kufurahia sana siku hiyo kwa sababu itakuwa ni Simba Day yangu ya kwanza," alisema Miquissone kabla ya mechi.

**JE, WAJUA?**



MAKIPA walionunuliwa kwa kitita kikubwa zaidi katika historia ya soka duniani; #5 Ederson Moraes (Manchester City - Euro milioni 40), #4 Andre Onana (Manchester United - Euro mililioni 52), #3 Gianluigi Buffon (Juventus - Euro milioni 53), #2 Alisson Becker (Liverpool - Euro milioni 62), #1 Kepa Arrizabalaga (Chelsea - Euro milioni 80).





# Serikali yamulika utendaji AZAKI za vijana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imezinyooshea kidole asasi za kiraia zinazojishughulisha na masuala ya vijana huku Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wakiagizwa kuzifanyia tathmini ili kujua utendaji kazi wake.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, aliagiza hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa wakati wa kongamano la vijana lililoandaliwa na asasi za kiraia 32 zinazojishughulisha na masuala ya vijana.

Katambi alisema ni lazima asasi zijulikane zinafanya nini ili kuona kama zinakidhi tija na haja ya vijana.

"Tujue kama zinakidhi tija na haja ya vijana wa taifa hili au ni kwa maslahi ya wachache. Lazima asasi zetu zote tutambue zinavyowagusa vijana, kuna asasi zipo ambazo hata mimi mwenyewe sijui hata zinafanya nini, ninaziona tu zipo," alisema.

Alimtaka Katibu Mkuu wa ofisi hiyo kwa kushirikiana na msajili wafanye tathmini ya haja na tija ya taasisi zilizosajiliwa za vijana ikiwa ni pamoja na kujua zinafanya nini na vikwazo vinavyowakabili.

"Mfanye tathmini ili kuhakikisha asasi hizo zinatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria na malengo ya serikali ili kuleta nafuu kwa vijana nchini," aliagiza.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Maendeleo ya Vijana mkoani Dodoma (DOYODO), Rajab Juma aliomba serikali kuzitengea ruzuku asasi zinazojihusisha na masuala ya vijana kama ilivyo kwa vyama vya siasa ili kuwafikia kundi kubwa la vijana katika kujenga kesho yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Freedom House, Daniel Lema, alisema bado kuna kundi la vijana wanashindwa kutumia fursa zinazowazunguka ili kutengeneza kipato na kuishia kulalamika huku Mkurugenzi wa Foundation For Civil Society, Francis Kiwanga, akisema lazima vijana wahamishe akili zao kutoka kulalamika na kutembea na vyeti wakisaka ajira, badala yake watumie fursa zinazowazunguka.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Prof. Adolf Mkenda (wa pili kushoto), akiwa na Balozi wa Morocco nchini, Zakaria El Goumori (kushoto), Balozi Liberata Mulamula (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Bank of Africa, Adam Mihayo (kulia), katika sherehe ya kuadhimisha Siku ya Morocco kumkumbuka Mfalme Mohammed wa VI iliyofanyika ubalozini jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DUWASA yaridhishwa utekelezaji mradi wa maji wa lita milioni 7.6

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BODI ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) imeridhishwa na utekelezaji wa mradi wa maji Nzuguni unaotajwa utapunguza makali ya mgawo wa maji kwa asilimia 11 jijini hapa.

Baada ya kukagua mradi huo, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Balozi Job Masima, alisema utazalisha lita milioni 7.6 kwa siku na kuongeza upatikanaji maji.

"Huu ni mradi muhimu sana na mkubwa ambao utabadilisha sura ya upatikanaji maji katika Jiji la Dodoma na mradi huu unatarajiwa kukamilika ndani ya mwezi huu, hivyo bodi imeona ni vizuri kuja kuona maendeleo na tumeridhika na maendeleo ya mradi huu," alisema.

Balozi Masima alisema kwa namna mradi huo ulivyo wanapata matumaini kuwa utakamilika ndani ya mwezi huu na kuzinduliwa mapema mwezi Septemba 2023, ili kutoa ahueni kwa wananchi kupata huduma ya maji.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Aron Joseph, alisema mradi huo hivi sasa umefikia asilimia 76 ya ujenzi na kwa mujibu wa mkataba unapaswa kukamilika ndani ya mwezi huu.

Alisema uwezo wa uzalishaji maji kwa sasa katika Jiji la Dodoma ni lita milioni 68 kwa siku, hivyo kukamilika kwa mradi huo kutaongeza hadi kufikia zaidi ya lita milioni 75 kwa siku.

# Halmashauri yabana watendaji wa vijiji mikutano mapato na matumizi

**Na Elisante John,** MKALAMA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida imewataka watendaji na viongozi ngazi ya vijiji kuitisha mikutano ya hadhara yenye vigezo stahiki kwa ajili ya kuwasomea wananchi taarifa ya mapato na matumizi ili kuondoa migogoro kati yao na wananchi. Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, James Mkwega, aliagiza hayo juzi wakati wa mkutano wa kawaida wa robo ya nne wa Baraza la Madiwani kwa mwaka wa fedha wa 2022/23. "Ili kumaliza tatizo la migogoro kati ya wananchi na viongozi, mikutano kuhusu taarifa ya mapato na matumizi, ninaomba sana kigezo kiwe wingi wa watu. Utakuta kijiji kina watu 3,000, lakini mahudhurio ni watu 80, hao ndio wawakatae kweli viongozi! Hii siyo sawa!

"Ninadhani Ofisa Utumishi uko hapa na unanisikia. Ninataka kuona na kuanzia sasa, ninahitaji takwimu za kila mkutano wa aina hii, mikutano yote ya kusomeana mapato na matumizi ni maalum na ni ya kisheria," aliagiza Mkwega.

Awali akiwasilisha taarifa ya fedha, Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Biashara wa halmashauri hiyo, Thadeus Mella, alisema kwa mwaka 2022/23, halmashauri ilikisia kukusanya mapato ya zaidi ya Sh. bilioni 26.5 toka vyanzo vyake vyote na hadi kufikia robo ya nne ya mwaka, zimekusanywa zaidi ya Sh. bilioni 22.6.

Hata hivyo, taarifa hiyo ilipokewa kwa mitazamo tofauti na baadhi ya madiwani, wakiwamo Mariamu Kahola na Bilali Msengi, walioitaka idara hiyo kutilia mkazo makusanyo yote yaliyoainishwa katika mpango mkakati wa mwaka wa fedha 2023/24 ili kuongeza mapato.





# Kilimo mawese kukuzwa kuzalisha mafuta kwa wingi

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa, amesema serikali inaendelea kufanya jitihada za kukuza kilimo cha alizeti ili nchi iweze kuzalisha kwa wingi mafuta ya kupikia na kuondokana na uhaba wa bidhaa hiyo.

Aidha, amesema moja ya taasisi ambazo zinashiriki katika jitihada hizo za serikali ni pamoja na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), ambalo limekuwa likizalisha zao hilo kwa wingi.

Bashungwa alisema hayo jijini hapa wakati akihitimisha ziara yake kwenye maonesho ya wakulima Nanenane katika viwanja vya John Mwakangale.

"Serikali inaendelea kufanya jitihada za kukuza kilimo cha alizeti, hata upade wa JKT inaendelea kuweka jitihada kubwa katika uzalishaji wa zao hilo ambalo faida zake ni nyingi ikiwamo kuokoa fedha za kigeni tunazotumia kuagiza mafuta nje ya nchi," alisema Bashungwa.

"Kwa hiyo mkakati wetu ndani ya serikali kupitia Jeshi la Kujenga Taifa ni kuongeza mawanda ya uzalishaji kupitia JKT maana kila mmoja hutumia mafuta haya, sasa kwa vile tumejaliwa ardhi nzuri na mikoa mingi zao hili linastawi vizuri basi JKT litakuwa mstari wa mbele kushirikiana na Wizara ya Kilimo kuongeza uzalishaji wa zao hilo na mazao mengine," alisema Bashungwa.

Aidha, JKT imesaini makubaliano na Wizara ya Kilimo ambayo yanaenda kuongeza tija katika shughuli za uzalishaji na kutoa mchango katika mageuzi ya kilimo nchini na kuzidi kutoa tija kwa wakulima.

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi zitashuhudia JKT likitiliana saini mkataba na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuhakikisha vijana wa JKT wanajengewa uwezo utakaowawezesha kujitegemea kupitia sekta za mifugo na uvuvi pindi wanapomaliza mkataba wao wa mafunzo ya JKT.

Alisema, hatua hiyo itaenda kusaidia vijana hao kujiajiri pia kuchangia katika Pato la Taifa.

"Takwimu zinaonesha asilimia 45 tu ya vijana wa kujitolea ndiyo wanapata ajira katika vyombo mbalimbali vya majeshi na asilimai 55 inayobaki wanarudi uraiani baada ya kumaliza mkataba wao JKT, sasa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan anataka kuona hiyo asilimia 55 ya vijana wanaohitimu mkataba wa kujitolea JKT inapata ajira," alisema Waziri Bashungwa.

Mkazi wa Mbeya, Aloyce John alisema kitendo cha sekta ya kilimo kushirikiana na JKT kimezidi kuongeza tija katika kilimo na wakulima wanakwenda kufanya kilimo chenye tija ambacho kitawainua kiuchumi.

Alisema pia anaishkuru serikali kutokana na kuwekeza kwenye sekta ya kilimo jambo linalozidi kuwashawishi wakulima wajikite katika kuendesha kilimo.

# Ukosefu vifaa, madaktari walazimisha wananchi kufuata huduma afya mbali

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

LICHA ya serikali kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Halungu, wilayani Mbozi mkoani Songwe, wananchi wa kata hiyo bado wanalazimika kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi kutokana na kituo hicho kukosa vifaa tiba, madaktari na wataalamu wengine wa afya.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara ambao uliandaliwa na Diwani wa Kata ya Halungu, Maarifa Mwashitete, baadhi ya wananchi walisema kuwa ukosefu wa madaktari na wauguzi kwenye kituo hicho cha afya unasababanishia kero ya kuendelea kusafiri umbali mrefu kufuata huduma wilayani.

Mkazi wa Kijiji cha Halungu, Rhoda Mwansyebela, alisema pamoja na serikali kujenga kituo hicho hawajaanza kunufaika kutokana na upungufu huo. "Tunaishukuru serikali kwa kutujengea kituo kizuri cha afya kwenye kata yetu, kwa kweli haya ni maendeleo makubwa ambayo yamefanyika, lakini kituo hiki hakina madaktari hivyo sisi kama wananchi hatujaanza kunufaika na uwekezaji huu," alisema Mansyebela.

Aliiomba serikali kukamilisha nia yake njema ya kuwajengea kituo hicho cha afya kwa kuwaletea wauguzi na vifaa tiba ili kianze kazi na kunufaisha.

Ben Mkwawa, mwananchi wa eneo hilo, alisema kuwa serikali imejitahidi kujenga miundombinu hiyo bora ya kituo cha afya kwa kutumia gharama kubwa na kwamba ni vizuri ikawaletea wataalamu wa afya ili adhima ya ujenzi wa kituo hicho ya kuwasogezea wananchi huduma za afya iweze kutimia.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Halungu, Moses Mshani, alisema serikali yake ya kijiji ilijitahidi kusimamia kwa makini miradi ya maendeleo waliyopelekewa na serikali ili ikamilike na kuwanufaisha wananchi.

Alisema, serikali pia imewezesha ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi Halungu na shule ya sekondari ya kata hiyo, miradi ambayo wameisimamia kwa karibu na imekamilika.

Diwani wa Kata ya Halungu, Maarifa Mwashitete, alisema serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi inachukua hatua za haraka za kutatua kero ya wananchi hao.

Alisema katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, imetenga bajeti ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kituo hicho. Aidha, alisema katika bajeti hiyo wanakusudia kununua vifaa tiba na kuvipeleka kwenye kituo hicho cha afya kabla ya kuwaleta wataalamu. "Hatujaleta hapa wataalamu wa afya kwa sababu bado hatujanunua vifaa tiba, maana wataalamu wakija bila kuwa na vifaa tiba bado hawawezi kutoa huduma kwa ufanisi, hivyo tunakusudia kwanza kuleta vifaa tiba na ndipo watalaam watakuja," alisema Mwashitete.

Alisema kuwa fedha zilizotengwa katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kituo hicho cha afya zitatumika kujenga majengo kwa ajili ya maabara na jengo la mionzi na kwamba yatakapokamilika kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kutoa huduma zote kama ilivyo kwenye hospotali ya wilaya na wananchi hawatakuwa na haja ya kusafiri kufuata huduma hizo wilayani.





Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Mkani Waziri (kushoto), alipotembelea banda la benki hiyo katika maonesho ya Nanenane yanaoendelea jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana wafundishwa kudhibiti sumukuvu kwenye mazao

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

VIJANA 420 kutoka mikoa 13 nchini wamefundishwa kudhibiti sumu kuvu ambayo kwa sasa imekuwa tishio baada ya mazao kuvunwa kwa kutengeneza vihenge vya chuma, lengo likiwa ni kumsaidia mkulima anapovuna na kukausha mazao yake ayahifadhi kwenye sehemu salama.

Mpango huo unafanywa kwa pamoja kati ya Mamlaka ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) na Wizara ya Kilimo ukiwa na lengo la kusaidia wakulima kuondokana na tatizo sumu kuvu kwenye mazao wakati wa mavuno.

Mratibu wa Mradi wa sumu kuvu kutoka VETA, Joseph Kimako, alisema hayo katika maonesho ya Nanenane kitaifa yanayoendelea katika viwanja vya John Mwakangale.

Kimako alisema katika mradi huo mamlaka hiyo inashughulika na kipengele cha baada ya kuvuna katika sehemu ya kuhifadhi na wakulima wamekuwa wakikabiliwa nalo kutokana na kukosa vifaa vya kuhifadhi kwa njia zinazokubalika.

Alisema vijana hao watakapomaliza mafunzo yao watapewa vifaa vya bure ili waweze kujiajiri kwa kutengeneza vihenge hivyo hasa katika maeneo ya wakulima wanaoishi kwenye vijiji.

"Lengo letu ni kuona tunamsaidia mkulima katika kupambana na sumu kuvu kwa sababu vijana watakuwa na nyenzo za kutengeneza vihenge kule kwenye mazingira yao," alisema Kimako.

Alisema mradi huo wa VETA umeingia makubaliano na Wizara ya Kilimo, katika eneo hilo la kuzuia athari ya sumukuvu kwenye mazao ya nafaka.

Naye Meneja Uhusiano wa Mamlaka hiyo, Sitta Peter, alisema wamekuwa wakitengeneza programu mbalimbali zinazolenga makundi mbalimbali ya kwenye jamii na kwenye kilimo.

"Mpango huu lengo lake ni kufanya uhifadhi wa mazao uwe ni bora kwa kutumia hivyo vihenge vya chuma, hivyo kudhibiti sumukuvu ambayo ina athiri mazao ya aina mbalimbali ikiwamo mahindi karanga na mazao mengine ya nafaka," alisema Sitta.

Alisema katika kilele cha maonesho ya Nanenane mkoani Mbeya, Rais Samia Suluhu Hassan, atagawa vifaa mbalimbali kwa hao vijana waliopata mafunzo ili waendelee kutengeneza vihenge mbalimbali vya chuma.



# Uanzishwaji ADRC kuleta mwelekeo mzuri uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

MWANASHERIA Mkuu wa Zanzibar, Dk. Mwinyi Talib Haji, amesema uanzishwaji wa Sheria na Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro nje ya Mahakama (ADRC) Zanzibar, kutaleta mwelekeo mzuri zaidi wa sekta ya uwekezaji na kuongeza imani ya wawekezaji kwa serikali.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo baada ya kupokea rasimu ya sheria ya usuluhishi wa migogoro pamoja na rasimu ya sheria ya uanzishaji wa kituo cha usuluhishi wa migogoro kutoka kwa mshauri elekezi, Dk. Alex Nguluma wa kampuni ya Rex Attorneys ya Dar es Salaam, hafla iliyofanyika Zanzibar.

Alisema kuwapo kwa sheria na kituo hicho Zanzibar ni jambo la lazima kutokana na kasi ya uwekezaji unaoendelea kufanyika nchini kote.

Alisema kituo hicho pia kinaakisi mtazamo mpana wa Rais wa Zanzibar katika dhamira yake ya kuimarisha na kurahisisha mazingira ya uwekezaji ili kukuza maendeleo nchini.

Alisema kituo hicho kitasaidia suluhu na maridhiano migogoro ya kibiashara na uwekezaji inapotokea na kuibakisha sekta ya uwekezaji nchini katika hali ya utulivu.

Mwakilishi wa Kampuni ya Rex Attorneys ya Dar es Salaam, Dk. Alex Nguluma, aliishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kuiamini taasisi yao na kuahidi ushirikiano ili kuhakikisha lengo la Serikali Kuu la kutaka kuanzisha sheria na kituo cha usuluhishi wa migogoro linatimia.

# Hekta 700 mikoko kupandwa kudhibiti mmomonyoko

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha mmomonyoko wa ardhi kwenye maeneo ya fukwe, jumla ya hekta 700 za miti aina ya mikoko zinatarajiwa kupandwa kisiwa cha Pemba ili kudhibiti hali hiyo.

Hayo yalisemwa visiwani Zanzibar na Mshauri mwelekezi wa mradi wa upandaji wa mikoko, Dk. Mwita Mangora, wakati wa utambulisho wa mradi huo wa matumizi endelevu ya miti hiyo katika ukanda wa Magharibi ya Bahari ya Hindi.

Alisema mradi huo baadhi ya malengo yake ni kudhibiti kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya juu ikiwamo katika makazi ya wananchi maeneo ya pembezoni mwa fukwe.

Mangora alisema baadhi ya maeneo ni tishio kwa athari za mazingira kutokana na kasi ya maji ya bahari kuja juu na kuingia katika maeneo ya makazi kutokana na kukosekana kwa baadhi ya miti.

"Mradi huu lengo lake kubwa kupambana na athari za mazingira katika maeneo ya fukwe za bahari pamoja na mmomonyoko wa ardhi kufuatia kujitokeza kwa kasi ya mabadiliko ya tabia ya nchi. Mkuu wa Wilaya ya Wete, Dk. Hamad Omar Bakari, alisema mradi wa kuotesha mikoko ni muhimu kutokana na kujitokeza kwa athari nyingi za mmomonyoko wa ardhi unaotokana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi.

Alisema hivi sasa baadhi ya maeneo katika kisiwa cha Pemba wananchi wameyakimbia kutokana na kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya fukwe na kusababisha athari kubwa.

Aliyataja maeneo yaliyoathirika ikiwamo kisiwa Panza pamoja na Mtambwe na wananchi wameanza kuyakimbia maeneo yao kutokana na baadhi ya maeneo ya fukwe kupata athari za mmomonyoko wa ardhi.

"Tunakabiliwa na changamoto kubwa za mmomonyoko wa ardhi unaotokana na mabadiliko ya tabia ya nchi ambapo athari zake tumeziona... njia pekee ya kukabiliana na tatizo hilo ni kuotesha miti aina ya mikoko pembezoni mwa bahari," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira, Sheha Mjaja Juma, alisema katika utekelezaji wa kurudisha Zanzibar ya kijani, wanatarajia kuotesha jumla ya miti ya mikoko milioni moja katika maeneo yaliopo pembezoni mwa bahari Unguja na Pemba.

Aidha, alisema wamepata faraja kubwa kupitia wamiliki wa hoteli nyingi za kitalii katika kufanikisha zoezi hilo na wameahidi kuunga mkono mapambano hayo kikamilifu.



Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed, akiwa pamoja na viongozi wa Wizara ya Kilimo kwenye maonesho ya Nanenane viwanja vya Dole Mkoa wa Mjini Magharibi ikiwa ni juhudi za kuunga mkono Siku ya Wakulima. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi asisitiza ushirikiano kiutendaji SMT, SMZ

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema ili kuendeleza mageuzi ya uchumi na uwekezaji lazima kuwapo na ushirikiano wa kiutendaji baina ya taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar alipozungumza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo na ujumbe wake wa watu 20 waliofika kujitambulisha. Alisema, SMZ na SMT wana ushirikiano mkubwa kwenye utendaji wa taasisi zao na kueleza mara kadhaa taasisi ya Hazina ya Zanzibar imekuwa ikipata ushirikiano mzuri na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar, ZIPA na TIC pamoja na taasisi nyingine za pande mbili hizo za Muungano hushirikiana katika kuboresha maendeleo kwa ustawi wa uchumi wa Taifa la Tanzania na watu wake.

Rais Dk. Mwinyi aliwapongeza na kuushukuru ujumbe huo kwa utayari wao kwa kuendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mawazo ya mageuzi yanayolenga kujenga uchumi wa wananchi wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia ushirikiano uliopo baina ya taasisi za serikali mbili hizo, zikiwamo Mamlaka ya Bandari, Ofisi ya Msajili Hazina, Mamlaka za uwekezaji pamoja na Tume ya Mipango ya Taifa.

"Niwapongeze kwa mawazo haya ya mageuzi, ni vizuri mara zote tuwe kunafikiria kujenga uchumi wetu kupitia taasisi zetu," alisema.

Akiizungumzia bandari jumuishi ya Mangapwaji, Rais Dk. Mwinyi, alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imepania kuleta mageuzi makubwa ya uchumi kupitia bandari hiyo, ambayo kutokana na maumbile ya kisiwa hicho kilivyo, inakusudiwa kujumuisha shughuli zote za bandari.

Alizitaja baadhi ya shughuli hizo ni kupakia na kushushia abiria na mizigo, lakini kuruhusu meli mbalimbali za kimataifa zitakazoleta mageuzi makubwa ya biashara, uwekezaji na kuimarisha uchumi wa buluu.

Naye Waziri Mkumbo alimwahidi Rais Dk. Mwinyi ushirikiano katika kuujenga uchumi wa nchi hasa kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanzania na ya Mapinduzi ya Zanzibar wamejipanga kuleta mabadiliko makubwa ya uchumi.

Alisema kupitia mradi wa Bagamoyo, ujio wa Zanzibar umewaletea tija na ufanisi mkubwa kwenye utendaji wao hasa kwa taasisi wanazoshirikiana nazo kiutendaji kwa kuwa watajifunza mengi kupitia bandari jumishi ya Mangapwani pamoja na taasisi nyingine wanazoshirikiana nazo kiutendaji. Ujumbe ulioongozana na Waziri Prof. Kitila umemjumuisha Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Dk. Tausi Kida, Msajili wa Hazina Bara, Nehemia Mchechu, Katibu wa Tume ya Mipango Lawrence Mafuru, Mkurugenzi Mkuu EPZA Charles Itembe, Mkurugenzi Mkuu TIC, Gilead Teri na Mkurugenzi wa Miundombinu TPA, Dk. Hussein Lufunyo.

# Panyabuku waleta tija unusaji majanga

**Na Christina Haule,** MOROGORO

TEKNOLOJIA ya matumizi ya panyabuku katika uokoaji kwenye majanga ya matetemeko ya ardhi, majengo na ajali imepongezwa kwa kuleta tija na manufaa nchini kutokana na kukabili vyema baadhi ya ajali ambazo awali zimechukua muda mrefu kwenye uokoaji na wakati mwingine kusababisha vifo visivyotarajiwa.

Mmoja wa wakazi wa Mkoa wa Morogoro waliohudhuria maonesho ya 30 ya wakulima 88 Kanda ya Mashariki, Lemeck Ponela, alisema jana kuwa amejifunza namna panya wanavyoweza kufanya shughuli za uokoaji wa miili iliyofukiwa kwenye vifusi baada ya kutokea majanga yakiwamo matetemeko ya ardhi, kuanguka kwa majengo na kubaini kuwa teknolojia hiyo itazaa matunda hapa nchini.

Awali, msimamizi wa mafunzo ya panya kutoka Taasisi ya Udhibiti viumbe waharibifu (PRPM & BTD) katika mradi wa Apopo uliopo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Pendo Msegu alisema hiyo ni hatua ya tatu ya miradi ya Apopo kwa panya buku kufanya shughuli za kusaidia kibinadamu na kuondoa dhana iliyojengeka kwa binadamu kuwa panya ni viumbe waharibifu muda wote.

Alisema katika awamu tatu ya tafiti zao kwa panyabuku wamegundua kuwa wana uwezo wa kusaidia serikali kuwaokoa watu wanaonasa kwenye vifusi wakati wa matetemeko ya ardhi au kuangukiwa na majengo na hivyo kuhakikisha wanapatikana kwa haraka na kupatiwa matibabu na pengine kuokoa uhai wao.

"Kwa kutumia uwezo wao mkubwa wa kunusa unaweza kutusaidia kugundua mengi zaidi, panya katika kuokoa watu kwenye athari za matetemeko ya ardhi tunaamini watafanya kazi vizuri kwa kuzingatia viwango vinavyotakiwa kulingana na mafunzo mazuri waliyopitia kuokoa maisha ya watu," alisema.

Aidha, Msegu alisema panya hao wana uwezo wa kupenya hata eneo ambalo binadamu hawezi kupenya na kuokoa watu waliofukiwa na kifusi baada ya tetemeko la ardhi kutokea huku wakiwa na kifaa maalum cha kufanyia kazi na wakibaini mwili wa mtu watabonyeza kifaa hicho na kumfanya mkufunzi kufuatilia na kutoa mwili huo.

Pia panya hao wanauwezo wa kuvaa kamera mgongoni ambayo itaonesha kama kuna nguo ya mtu au mtu amefukiwa na msimamizi wa mafunzo atakuwa na anaangalia kwenye kompyuta itakayokuwa ikimwonesha yule panya na kuweza kumwokoa mtu atakayeonekana kwenye kamera kwa haraka.

Alisema panya hao pia hutumika kwenye maeneo ya usafirishaji ikiwamo viwanja vya ndege au bandari na kuisaidia serikali kukamata wahalifu wanaojaribu kutoroka baada ya kuchukua nyara za serikali kwa njia ambayo sio halali.

Alisema tayari walishafanya kazi kwa kutumia panyabuku kwenye nchi za Msumbiji, Angola, Kambodia na kwingine kwenye eneo la ugonjwa wa kifua kikuu na panya kuwa na uwezo mkubwa na kusaidia kugundua ugonjwa huo na watu kupatiwa tiba mapema.

Ili panya wafanye kazi vizuri wanazingatia vigezo vya haki za wanyama kwa kuwatunza mahali pazuri, kula vizuri na wakiumwa huwapatia matibabu, vifaa na muda wa kufanya mazoezi ikiwamo kuruka kamba na kupanda ngazi ili kufanya miili yao iwe imara na kufanya kazi vizuri wanapohitajika.

Alisema panya hao wanapofikia miaka saba hustaafu na hupewa nyumba maalum na huduma muhimu na hutunzwa mpaka mwisho wa uhai wao ambao ni miaka tisa hadi 10 tofauti na panya wa porini ambao hufariki katika umri wa miaka miwili kutokana na kukosa matunzo.

Mwalimu wa panya hao, Mariam Chamkwata, alisema kupitia mradi wa Apopo kwenye teknolojia ya kubaini vimelea vya kifua kikuu (TB) katika mwaka 2022 watu 71,000 walibainika kuwa na ugonjwa huo na kupatiwa matibabu kwa haraka.

Alisema kupitia panya buku hao wana vituo 71 mpaka sasa vya kutolea huduma na wanafanya kazi na hospitali za rufani katika mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Pwani na Dodoma.

Chamkwata alisema mgonjwa mmoja ambaye hakupatiwa matibabu anaweza kuambukiza watu 18-20 kwa mwaka kwa njia ya hewa, lakini kwa kutumia panya buku ni faida kwa sababu ana uwezo wa kutoa majibu ya ugonjwa haraka tofauti na mashine za hospitali ambazo humtaka mgonjwa kupimwa TB kwa kupeleka makohozi mara tatu ambayo huchukua muda mrefu kutoa majibu.



Mkurugenzi wa Shirika la Kijerumani la Heinrich Boell Stiftung (HBS) lenye makao makuu jijini Nairobi Kenya ambalo linafanya shughuli zake katika nchi za Kenya, Tanzania na Uganda, Joachim Paul (kulia), akiweka shada la maua katika mnara wa Kumbukumbu ya Mangi Meli wa Old-Moshi ambaye aliuawa kwa kunyongwa na wakoloni wa Kijerumani Kolila, wilayani Moshi vijijini mkoani Kilimanjaro Machi 2, mwaka 1900. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kisare Makori. **PICHA: JAMES LANKA**

# Waziri Mkuu apongeza mikopo zana za kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezitaka taasisi za fedha nchini kuendelea kubuni huduma zinazolenga kutatua changamoto zinazowagusa wakulima, akipongeza hatua ya Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kuwekeza nguvu katika utoaji wa mikopo ya zana za kilimo kwa wakulima.

Majaliwa alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipotembelea banda la NBC katika Maonesho ya Kilimo Nanenane yanayoendelea kwenye Viwanja vya John Mwakangale mjini Mbeya.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa zana za kilimo, utasaidia kuchochea mapinduzi ya kilimo kwa kuchochea kasi ya uzalishaji na ongezeko la mapato kwa wakulima.

"Siku zote serikali imekuwa ikisisitiza na kuziomba taasisi mbalimbali za kibenki kuongeza juhudi katika ubunifu wa huduma zake ili zije na huduma zinazoonekana kutatua kero za makundi mbalimbali kulingana na mahitaji yao mahususi.

"Na hii ndiyo sababu ninawapongeza Benki ya NBC ambao kupitia mkakati wa NBC Shambani wanaweza kuwasaidia wakulima wengi kupata mikopo ya zana muhimu za kilimo... hongereni sana NBC," Waziri Mkuu alipongeza.

Awali akifafanua kuhusu mikopo hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo, Lariba na wakulima kutoka Benki ya NBC, Raymond Urassa alisema kupitia ushirikiano na kampuni ya kuuza pembejeo za kilimo ya Agricom Africa, benki hiyo tayari imefanikiwa kutoa mikopo ya zana za kilimo zenye thamani ya Sh. bilioni 2.3 kwa wakulima mbalimbali nchini.

"Hatua yetu hii ni mwendelezo tu wa jitihada zetu nyingi tunazozielekeza katika sekta ya kilimo ili kuunga mkono juhudi za serikali katika kuinua sekta ya kilimo nchini," alisema Urassa.

Katika kuthibitisha dhamira hiyo, benki hiyo mwishoni mwa wiki ilikabidhi mkopo wa trekta na majembe vyenye thamani ya Sh. milioni 62.1 uliotolewa kwa mkulima wa mpunga Evarist Msasi kutoka wilayani Mbarali, mkoani Mbeya.

Urassa wakati wa makabidhiano hayo, alibainisha kuwa tangu walipoingia ubia na kampuni Agricom, NBC imeshawezesha kuwapatia wakulima mikopo ya matrekta 20, mitambo ya uvunaji (combiner harvester) 15 na power tiller 10.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Saddy Kambona, aliipongeza NBC pamoja na Agricom Africa kwa kuunga mkono juhudi za serikali katika kuinua sekta ya kilimo nchini.

## Sababu wahitimu kukosa ajira serikalini zaanikwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** MBEYA

SEKRETARIETI ya Ajira katika Utumishi wa Umma imetaja sababu za wahitimu wengi kukosa ajira serikalini kunatokana na vyuo vingi nchini kuwa na tabia ya kuanzisha kozi mpya ambazo haziendani na miundo ya maendeleo ya utumishi kwa lengo la kupata wanafunzi wengi na kuongeza mapato.

Katibu Msaidizi wa Sekretarieti ya Ajira, Somwana Manjenga, akizungumza jana katika mahojiano na Nipashe kwenye maonesho ya wakulima na wafugaji Nanenane yanayofanyika viwanja vya John Mwakangale jijini hapa, alisema tatizo hilo limekuwa sugu na kusababisha wahitimu wengi kukosa ajira kutokana na kozi walizosomea kutoendana na miundo ya maendeleo ya utumishi.

Manjenga alitoa mfano kada ya upishi ambayo inataka ili mtu aweze kuajiriwa kuwa mpishi lazima awe amesomea kozi ya 'Food Production' kwa ngazi ya cheti, shahada au diploma lakini hivi sasa vyuo vimeanzisha kozi mpya iitwayo 'Culinary Art' ambayo inafanana na kozi ya food production lakini kwenye mfumo haitambuliki kwenye miundo ya maendeleo ya utumishi.

Alisema kwa kuwa changamoto hiyo inajitokeza sana na kuzua malalamiko kwa wananchi na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora ambayo inahusika na miundo ya maendeleo ya utumishi imeziandikia barua wizara ili zirekebishe na kuhuisha miundo yao ili iendane na soko la ajira lililopo mitaani.

Kwa upande wa vyuo, alisema Sekretarieti ya Ajira imekuwa ikivishauri vinapoanzisha kozi mpya au marekebisho ya mitaala iwe inaishirikisha ili Sekretarieti ya Ajira iweze kutoa maoni kuwa na kozi ambazo zinatambulika katika miundo ya maendeleo ya utumishi.

# Mbeya kunufaika mradi kopa ng'ombe lipa maziwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema wizara yake kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo watapeleka mradi wa 'Kopa Ng'ombe Lipa Maziwa' kwa wananchi wa Mkoa wa Mbeya vijijini ili kuwawezesha vijana na kinamama kujikwamua kimaisha.

Waziri Ulega (pichani chini) aliyasema hayo alipofanya ziara kwenye Halmashauri ya mji mdogo, Mbalizi, Wilaya ya Mbeya, mwishoni mwa wiki.

"Mbunge wenu ameniomba mambo mengi ikiwa pamoja na kuifanya Mbeya kuwa ni eneo la kielelezo la kufuga kisasa na kibiashara, hivyo, nitawatafutia mradi mzuri wa Kopa Ng'ombe Lipa Maziwa, Mbunge nataka uwatafutie uchumi watu wa hapa Mbeya," alisema Ulega.

Waziri Ulega alimwelekeza Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, kufika katika Ofisi za Shirika la Heifer International na Benki ya Maendeleo ya Kilimo ya (TADB), mkoani humo kwa ajili ya kuanza taratibu za kuwezeshwa kupata mradi huo huku akimuahidi kuwa atahakikisha wananchi wa Mbeya vijijini wanapata mradi huo ili waweze kunufaika nao.

Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, alimshukuru waziri Ulega kwa kuwapelekea mradi huo ambao alisema amewapelekea utajiri wananchi wa Mkoa Mbeya.



# Amchoma mikono mwanawe kisa kudokoa mboga jikoni

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKAZI wa Changamati wilayani Sengerema, Maneno Thomas (35), anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani humo kwa tuhuma za kumchoma mikono na maji ya moto mwanawe kwa madai ya kudokoa mboga za majani.

Mwanamume huyo anayedaiwa kukimbiwa na mkewe hivi karibuni kutokana na vitendo vyake vya kikatili vikiwamo vipigo vya mara kwa mara, anadaiwa kutekeleza ukatili huo Agosti 2, mwaka huu, majira ya saa mbili usiku.

Prisca Maneno (11) binti ya mwanamume huyo, alidai kuwa siku ya tukio baba yao alirejea kutoka kazini majira ya saa mbili na kumuomba amwandalie chakula na yeye alimwambia kuwa hakukuwa na mboga, iliyokuwapo ililiwa na mdogo wake (jina tunalo) mwenye umri wa miaka tisa mvulana anayesoma darasa la pili.

Alisema baada ya kumwambia hivyo baba yake, aliingia jikoni na kuwasha moto kisha kuchemsha maji na kumuita mwanawe aliyedaiwa kula mboga na kisha kumwagia maji ya moto kwenye mikono yote.

Baada ya kumsababishia maumivu hayo alimfungia ndani ya chumba kwa lengo la kumficha asionekane na majirani kwa kuwa alikuwa ameungua vibaya mikononi.

Akithibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo juzi, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilbroad Mutafungwa, alisema baada ya uchunguzi uliofanywa na majirani na kubaini kuwa mtoto amefanyiwa ukatili huo waliamua kumweka kizuizini bila kuchukua sheria mkononi.

"Waliona mtoto huyo hatoki ndani kwa muda wakashangaa na walipogundua kitendo hicho wakamkamata na kutoa taarifa katika kituo cha polisi ambapo mtuhumiwa huyo alikiri kutenda ukatili huo kwa kile alichosema ni hasira," alisema SACP Mutafungwa.

Alisema, hali ya mtoto inaendelea vizuri baada ya kupelekwa kituo cha afya cha Kamanga na kuendelea kupatiwa matibabu huku mtuhumiwa akitarajiwa kufikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

"Tunawapongeza wananchi na wakazi wa Kijiji cha Kamanga, Kata ya Nyamatongo wilayani Sengerema kwa kupinga ukatili na kutojichukulia sheria mkononi wakati wa kumkamata mtuhumiwa," alisema.

Aliwataka wananchi kuendelea kuwa na falsafa ya polisi jamii na ulinzi shirikishi kwa kutokuficha taarifa za uhalifu na wahalifu ili kuisaidia polisi kutekeleza majukumu yao.



Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma (kulia), akimsikiliza Mkurugenzi wa Kampuni ya Franone Mining and Gems LTD, Onesmo Mbise (kushoto), alipotembelea mgodi wa madini ya Tanzanite Kitalu C, Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro juzi, (wa pili kulia) ni Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga. **PICHA: GIFT THADEY**

# Benki ya Exim yajivunia faida ya bilioni 36.6/-

**Na Halfani Chusi**

BENKI ya Exim imepata faida ya Sh. bilioni 36.6 kabla ya makato ya kodi kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo wa mwaka huu ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.9 kwa mujibu wa taarifa ya fedha ya benki hiyo.

Kutokana na mafanikio hayo, uongozi wa benki hiyo umesema utaendelea na dhamira yake ya kuwekeza katika teknolojia ya kisasa ili kuboresha utoaji huduma kwa wateja katika matawi yake ndani na nje ya Tanzania.

Kwa mujibu wa Ofisa Mkuu wa Fedha wa benki hiyo, Shani Kinswaga, benki hiyo mwanzoni mwa mwaka huu iliboresha mfumo wake na kuweka miundombinu thabiti, hatua inayolenga kuimarisha utendaji wake na kuwapa wateja hali ya juu ya usalama, ufanisi na uvumbuzi.

"Hii inadhihirisha ari yetu katika kubadilika na kuwa zaidi ya taasisi ya benki. Kama benki, tumejitolea kuwekeza katika kuongeza uwezo wa mifumo yetu ili kutoa huduma bora kwa wateja wetu na jamii inayotuzunguka," Kinswaga alisema.

Ofisa huyo katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana alisema matokeo ya benki hiyo kwa kipindi cha miezi sita ya kwanza mwaka huu yanadhihirisha dhamira ya benki hiyo ya kufanya kazi kwa ufanisi kufuatia utekelezaji wa mkakati wa benki hiyo kimamilifu ili kunufaisha wadau wote wa benki hiyo na jamii kwa ujumla.

Mapato ya benki hiyo yenye matawi nje ya Tanzania katika nchi za Comoro, Djibouti na Uganda, yaliongezeka kwa asilimia 9.6 hadi kufikia Sh. bilioni 66.2 kwa miezi sita iliyoishia tarehe 30 Juni 2023 kulinganishwa na Sh. bilioni 60.4 zilizopatikana katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Kinswaga alisema mazingira mazuri ya biashara yalichangia katika utendaji mzuri wa kifedha na kiutendaji wa benki katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka huu wa 2023.

Kinswaga alisema amana za wateja wa benki hiyo kufikia Juni 30, 2023 ziliongezeka kwa asilimia 9.2 hadi Sh. trilioni 1.9 huku mfuko wa wanahisa nao ukiongezeka kwa asilimia 23.9 hadi kufikia Sh. bilioni 291 kulinganishwa na kipindi kama hicho mwaka jana.

Mapato ya benki hiyo Isiyofadhiliwa (NFI) yalikua kwa asilimia 24.8 hadi kufikia Sh. bilioni 45.3 huku ufadhili wa mikopo ukiongezeka kwa asilimia 11.11 hadi kufikia Sh. trilioni 1.3 kulinganishwa na kipindi kama hicho mwaka jana.

Ofisa Mkuu Mtendaji wa benki hiyo, Jaffari Matundu, alisema benki hiyo ilichukua hatua madhubuti kuimarisha utendaji kazi wake kwa kuzingatia usalama, ufanisi na uvumbuzi katika huduma zao huku benki hiyo ikiboresha miundombinu yake.

Matundu alisema benki katika kipindi cha miezi sita ya kwanza mwaka huu iliendelea kutekeleza mkakati wake wa Uwekezaji wa Kijamii (CSI) kutokana na dhamira yake ya kuleta maendeleo endelevu kupitia programu mbalimbali za Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) zinazolenga thamani kwa wadau wake ikiwamo jamii ambazo benki inaendesha shughuli zake.

## HABARI MICHEZO

# DABO AKERWA KIWANGO AZAM FC KUELEKEA NGAO YA JAMII

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC imeinasa saini ya winga wa Azam FC, Tepsi Evance, kwa mkopo wa mwaka mmoja na tayari mchezaji huyo amejiunga na kambi ya timu hiyo.

**Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo, imeeleza kuwa wameingia mkataba wa mwaka mmoja na mchezaji huyo akitokea Azam FC, ikiamini atakuwa msaada mkuba kwenye kikosi hicho.**

"Tuna furaha kuwataarifu kuwa tumeingia mkataba wa mwaka mmoja na Tepsi Evance akitokea Azam FC kwa mkopo," ilieleza taarifa hiyo.

KMC inaonekana kufanya usajili mkubwa kuelekea msimu ujao wa ligi baada ya kutofanya vema msimu uliopita.

Tayari imeshawasajili Rogers Gabriel kutoka Pamba na Juma Shemvuni, Wibol Maseke aliyeachwa na Azam FC, Rahim Shomari na Andrew Sinchimba, ikimtwaa pia straika Ibrahim Elias raia wa Somalia kutoka Klabu ya Kibra United ya Kenya.

Hivi karibuni, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala, alisema kuwa kimetengwa kiasi cha Sh. bilioni moja kwa ajili ya usajili wa msimu unaokuja na hawatosajili mchezaji yeyote ambaye ameachwa na klabu yake.

"Mkurugenzi wetu mama Hanifa Selemani Hamza, ametenga kiasi cha Sh. bilioni moja kwa ajili ya kufanya usajili, maisha magumu tulioyapitia kwa msimu miwili iliyopita haikuwa rafiki kwetu, lazima tufanye usajili wa maana na kwa pesa hizi KMC hatusubiri wachezaji makapi, sijui nani kaachwa ndiyo tuende kumsajili.

"Msimu huu hatuchukui wachezaji ambao wameshindwa kufanya vizuri walikotoka, badala yake ni wapya kabisa kwenye macho ya mashabiki wa soka nchini na wengine tutawavunjia mikataba kwenye klabu zao na kuwasajili," alisema.

Wakati huo huo, KMC juzi ilicheza mechi ya kujipima nguvu dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro na kushinda mabao 6-4 kwa mikwaju ya penalti, baada ya sare ya bao 1-1 dakika 90 za mchezo.

# JKT Tanzania yataka ya JKT Queens

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya JKT Tanzania ambayo imerejea tena Ligi Kuu, imesema lengo lao kwenye Ligi ya msimu wa 2023/24 ni kuzisaka nafasi nne za juu lengo likiwa ni kucheza michuano ya kimataifa na si kupigania ili isishuke daraja kama ilivyokuwa ikifanya huko nyuma kabla haijashuka.

Akizungumza juzi baada ya ushishi wa bao 1-0 dhidi ya Stand United ambayo nayo inajiandaa na Ligi ya Championship baada ya kupanda kutoka 'First League', Kocha Msaidizi wa timu hiyo, George Mketo, alisema wanatambua msimu ujao utakuwa mgumu, lakini na wao wamejizatiti kwa kufanya usajili bora ambao utawafanya kupigania nafasi nne za juu ili kusaka tiketi ya kucheza kimataifa kama ambavyo timu yao ya Wanawake, JKT Queens imefanya msimu uliomalizika kwa kutwaa ubingwa na itacheza michuano ya CECAFA kusaka nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika.

JKT Tanzania iliyopiga kambi Shinyanga kwa ajili ya 'pre season', ilicheza mechi hiyo kwenye Uwanja wa Kambarage dhidi ya Stand United yenye maskani yake mjini humo.

"Tumeshacheza mechi tatu hapa, ya kwanza tumetoka sare na Kagera Sugar bao 1-1, ilikuwa ngumu na nzito, tumecheza na Kombaini ya Shinyanga, tumetoka sare ya mabao 2-2 na leo (juzi) tumecheza na Stand United tumepata ushindi wa bao 1-0, sisi kwetu matokeo si muhimu sana kwa sasa, ila tunaangalia jinsi gani wachezaji wetu wanafanya kile ambacho tumewaelekeza na kama wanakifanya kwa usahihi," alisema Mketo.

Hata hivyo, zipo taarifa kuwa huenda timu hiyo ikaweka makazi yake hapo na kucheza mechi zake za Ligi Kuu Uwanja wa Kambarage Shinyanga.

## MTANISOMA TU...



Kiungo na mshambuliaji wa Simba, Willy Essomba Onana, na mfungaji wa bao la kwanza kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Power Dynamos ya Zambia, akisalimia mashabiki wakati wa utambulisho wa wachezaji kwenye Tamasha la Simba Day lililofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Dodoma Jiji yataka kama Mashujaa FC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji imewaomba mashabiki wa timu hiyo kuiunga mkono wakati popote pale, itakapoanza kucheza mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/24.

Kocha Msaidizi wa klabu hiyo, Kassim Liogope amesema pamoja na kwamba wanafanya mazoezi makali ya kukiandaa kikosi kwa msimu ujao wa ligi huku wakiwa wametengeneza kikosi bora, lakini yote hayo hayaweza kufanikiwa kama hawatopata sapoti kutoka kwa mashabiki wa soka wa timu hiyo waliopo jijini Dodoma.

Aliwataka kujitokeza kwa wingi kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma wakati watakapoanza kucheza, lakini kuwasapoti wanapokwenda ugenini kama ambavyo walivyokuwa wakifanya mashabiki wa Mashujaa FC ya Kigoma wakati wakiipigania timu yao ipande Ligi Kuu na hatimaye kufanikiwa.

"Kikubwa waendelee kutusapoti tunajua msimu uliopita hatukuanza vizuri, lakini tuliwapoza kwa kile ambacho tuliwapa kwenye mechi za mwisho, hivyo tunaahidi kuendeleza pale tulipoishia, ile nguvu tuliomaliza nayo naamini ndiyo tutaanza nayo na nadhani itakuwa zaidi ya ile, najua kwa sasa wana hamu na timu yao wasubirie tu tukirudi Dodoma watakapa kile wanachotarajia," alisema Liogope.

# Kocha wa Taifa U-18 Zanzibar aona tofauti

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Timu za Taifa za Wanawake Zanzibar, Abdul Mutik Ali, amesema licha ya timu ya Wasichana chini ya umri wa miaka 18, kutofanya vizuri katika michuano ya Cecafa, imepiga hatua kubwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema timu hiyo ilionesha ushindani wa hali ya juu na wachezaji walipambana kwa kujiamini ikilinganishwa na ilivyozoeleka kwa upande wa timu za Wanawake za Zanzibar.

Alisema katika michuano hiyo ambayo ni kwa mara ya Kwanza Zanzibar inakuwa na timu ya wasichana, licha ya kutopata ushindi katika michezo yote minne waliyocheza, lakini kulikuwa na utofauti mkubwa hasa katika viwango vya wachezaji walivyoonesha kwenye michuano hiyo.

"Kwa mara ya Kwanza tumefanikiwa kuunda timu ya wasichana chini ya umri wa miaka 18, lakini wamefanya vizuri ikilinganishwa na ilivyozoeleka, hii inatupa mwanga wakujua wapi tuanzie katika timu hizi," alisema.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LAPORTE AWANIWA CITY

KLABU ya Manchester City wanatafuta fedha za kumnunua mlinzi wa Hispania, Aymeric Laporte mwenye umri wa miaka 29, baada ya kumsajili beki wa kati wa Croatia mwenye umri wa miaka 21, Josko Gvardiol kutoka RB Leipzig. ***(Mirror)***

### LEVY AIPUUZA BAYERN

MWENYEKITI wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy amewapuuza Bayern Munich kufanya uamuzi kuhusu ombi lao la pauni milioni 86 kwa mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 30. ***(Bild - in German)***

### KUDUS SAFI BRIGHTON

KLABU ya Brighton wamekubali mkataba wa kumnunua kiungo wa kati wa Ajax na Ghana, Mohammed Kudus, 23, kwa ada ya pauni milioni 34.5. ***(Athletic)***

### PHILOGENE ALENGWA LEVER

WINGA wa Aston Villa, Jaden Philogene, 21, ameonekana kulengwa na Liverpool. ***(Liverpool Echo)***

### ZANIOLO AWANIWA

KLABU ya Newcastle United wamekuwa wakiwasiliana na wakala wa mshambuliaji wa Galatasaray, Nicolo Zaniolo, 24, lakini AC Milan na Juventus pia zinavutiwa na mchezaji huyo wa Kimataifa wa Italia. ***(Chronicle)***

### COUTINHO AMULIKWA QATAR

KLABU ya Qatar ambayo haikutajwa jina imewasiliana na Aston Villa kuhusu kupatikana kwa kiungo wa kati wa Brazil, Philippe Coutinho, 31. ***(Fabrizio Romano)***

### OLISE, CHELSEA KIMEELEWEKA

CHELSEA imefikia makubaliano binafsi na winga Mfaransa, Michael Olise, 21, baada ya kuipa Crystal Palace pauni milioni 26. ***(Metro)***

### TOPSOBA APOTEZEWA SPURS

MLINZI wa Bayer Leverkusen na Burkina Faso, Edmond Tapsoba, 24, halengwi tena na Tottenham kwani wanaelekeza nguvu zao katika kumsajili beki wa kati wa Wolfsburg, Mholanzi Micky van de Ven, 22. ***(Yahoo)***

### PALACE JICHO KWA HALL

MLINZI wa Kimataifa wa England chini ya umri wa miaka 21, Lewis Hall, 18, anaweza kuruhusiwa kuondoka Chelsea kwa mkopo, huku Crystal Palace wakimsaka. ***(Dakika 90)***

### SCHMEICHEL NA NOTTINGHAM

KLABU ya Nottingham Forest imeanza mazungumzo na Nice kuhusu kumnunua mlinda mlango wa Denmark, Kasper Schmeichel, 36. ***(Nottingham Post)***

### BALOGUN ANUKIA MIAMI

INTER Milan wanamtaka mshambuliaji wa Arsenal, Folarin Balogun, 22, baada ya kumkosa mshambuliaji wa West Ham na Italia, Gianluca Scamacca (24), ambaye anaelekea kujiunga na Atalanta. ***(Express)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HØJLUND SASA RASMI MALI YA MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER imemsajili mshambuliaji, Rasmus Højlund, kutoka Atalanta kwa mkataba wa miaka mitano, klabu hiyo imetangaza.

**ESPN iliripoti mwezi uliopita kwamba United walikuwa tayari kulipa pauni milioni 64 pamoja na nyongeza nyingine ya pauni milioni nane kwa mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 20.**

Kocha wa United, Erik ten Hag, amekuwa na nia ya kuimarisha chaguo lake kabla ya msimu ujao huku klabu hiyo ikiamua kumuangazia Højlund baada ya kushindwa kwenye mbio za kumwania Harry Kane na Victor Osimhen.

"Si siri kwamba nimekuwa shabiki wa klabu hii kubwa tangu nikiwa mvulana mdogo, na nilikuwa na ndoto ya kutembea nje ya Old Trafford kama mchezaji wa Manchester United," alisema Højlund.

**●●● Nimefurahishwa sana na nafasi hii ya kugeuza ndoto hiyo kuwa kweli na nimedhamiria...**

"Nimefurahishwa sana na nafasi hii ya kugeuza ndoto hiyo kuwa kweli, na nimedhamiria kulipa imani ambayo klabu imeonesha kwangu. Bado ni mapema katika maisha yangu, lakini najua niko tayari kufanya hili."

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba wakati Ten Hag hapo awali alipendelea kuongeza mshambuliaji mwenye uzoefu kwenye kikosi chake, Mholanzi huyo amekuja na wazo la kufanya kazi na kijana Højlund kwa sababu ya uwezo wake.

"Mara tu nilipozungumza na kocha nilijua kuwa mazingira haya yangekuwa bora kwa maendeleo yangu," alisema Højlund.

"Ninafurahia fursa ya kufanya kazi na mmoja wa makocha bora duniani. Chini ya uongozi wake na usaidizi, najua kwamba nina uwezo wa kufikia mambo makubwa pamoja na wachezaji wenzangu wapya katika klabu hii maalum."

Højlund alifunga mabao tisa katika mechi 32 akiwa na Atalanta kwenye Serie A msimu uliopita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark ndiye mchezaji wa hivi karibuni kusajiliwa na United msimu huu wa majira ya joto kufuatia kuwasili kwa kiungo Mason Mount kutoka Chelsea na kipa André Onana kutoka Inter Milan.

Mkurugenzi wa soka wa United, John Murtough alisema: "Katika kipindi chote cha majira ya joto tumechukua hatua za haraka na madhubuti ili kufikia malengo yetu ya msingi mapema katika dirisha la usajili. Hii itahakikisha kwamba Erik na makocha wake wanapata fursa nzuri zaidi ya kukiandaa kikosi ili kusukuma mbele mafanikio zaidi."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
SV DARMSTADT
1 | 1.32
X | 5.31
2 | 6.54

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# POCHETTINO ATAKA CHELSEA KWA LIVER



**NEW YORK,** Marekani

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Mauricio Pochettino, amesisitiza kuwa analenga mafanikio ya haraka katika klabu hiyo, lakini akasisitiza kwamba anahitaji muda kujenga msingi wa kufanyia kazi.

Klabu hiyo ya London Magharibi inaingia katika msimu wao wa pili kamili chini ya umiliki wa Todd Boehly na BlueCo, kuelekea kwenye kampeni mpya baada ya kampeni mbaya kabisa msimu uliopita.

'The Blues' hao walipitia kwa makocha wanne na kumaliza katika nafasi ya 12 - ikiwa ni nafasi mbaya zaidi tangu msimu wa 1993/94.

Akizungumza na Evening Standard wakati wa kuhitimisha ziara yao nchini Marekani, Pochettino alieleza kuwa Chelsea wanapaswa kuzingatia kufuata mifano ya Liverpool, Manchester City na Real Madrid katika kupanga mipango ya muda mrefu ya kufanikiwa.

"Huwezi kushinda ikiwa hautajenga," alisema Pochettino. "Unaweza kuleta majina na wachezaji...kuna tofauti, lakini kwa ujumla klabu zote zinashinda kwa mipango. "Liverpool ilishinda baada ya miaka mingi kufanya kazi kwa bidii na kuwa na msimamo, Manchester City sawa baada ya miaka saba au nane na Pep Guardiola na Real Madrid pia.

"Hilo ni muhimu kuelewa, klabu zinavyoshinda ni timu ambazo zina msimamo zaidi, zinazofanya kazi kwa bidii kutengeneza mpango wa kushinda. Kazi yetu ni kuipa timu utulivu wakati wa kupanda na kushuka, kuwa na tabia sawa."



## Man City yainasa saini ya Gvardi

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City wamepiga hatua kubwa zaidi katika dirisha la usajili la majira haya ya joto kwa kumsajili beki wa kati, Josko Gvardiol kutoka RB Leipzig.

Vyanzo viliiambia ESPN mapema wiki hii klabu hizo zimeikubali ada ya euro milioni 90 kwa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Croatia bila nyongeza.

Hapo awali Leipzig walikuwa wamemthaminisha Gvardiol kwa euro milioni 100, msimamo ambao ulizuia mazungumzo mapema msimu huu wa majira ya joto.

Thamani ya Leipzig ingemfanya Gvardiol kuwa beki ghali zaidi duniani, lakini ada ya mazungumzo ya City ni chini ya ambayo Manchester United ililipa Leicester City kwa Harry Maguire mwaka 2019.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, alijiunga na Leipzig kwa ada ya karibu euro milioni 19 mwaka 2020 na baada ya kukaa kwa mkopo kwa msimu mmoja huko Dinamo Zagreb, alijidhihirisha kama mtu muhimu.

Ameichezea Croatia mechi 21 na alikuwa sehemu ya timu iliyomaliza nafasi ya tatu kwenye Kombe la Dunia la mwaka 2022 nchini Qa

Gvardiol ni mchezaji
pili kusajiliwa na City ms
huu wa majira ya joto ba
ya kuwasili kwa mche
mwingine wa Kimataifa
Croatia, Mateo Kovacic,
ada ya awali ya pauni mil
25 kutoka Chelsea.

Tangu kikosi cha
Guardiola kinyanyue m
matatu msimu uliopita, I
Gündogan na Riyad Mal
wote wameondoka na b
kunaweza kuwa na wa
zaji wengine wanaoond
huku Bernardo Silva,
Walker, Kalvin Phillips
Aymeric Laporte wakita
kuwaniwa sehemu nyingi

## HABARI MICHEZO


Y | CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU,
BET LEO UWE MILIONEA




# SKUDU AWAITA YANGA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha Yanga kikiondoka leo kuelekea Tanga kwa ajili ya mechi ya Ngao ya Jamii, itakayopigwa Uwanja wa Mkwakwani Jumatano dhidi ya Azam FC, winga mpya machachari wa timu hiyo, Mahlatse Makudubela 'Skudu', amewataka wanachama na mashabiki kuminimika kwa wingi Uwanja wa Mkwakwani ili kupata burudani safi pamoja na ushindi.

Wakati akiongea hayo jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamondi amesema wachezaji wake wako tayari na mechi hiyo, ingawa kuna changamoto ya kuboresha miili ya baadhi ya wachezaji ambao wamechelewa kujiunga na wenzao kambini.

**Skudu alisema wapo vizuri kimwili na kiakili na hawaangalii mpinzani anafanya nini bali wataangalia wao watakavyowapa furaha mashabiki.**

"Tumekuwa tukifanya kazi kubwa, wachezaji wanaonekana kuwa na kasi na wepesi, tunasubiri tuanze kucheza na tutaanza na Ngao ya Jamii, tupo vizuri kwa kushinda na tutawashangaza, hatuwatazami wapinzani wetu tunajitazama sisi, unajua tumefanya kazi nzuri tupo tayari kiakili na kimwili.

"Tunasubiri siku ifike, unajua nimejifunza kuwa tunapocheza wanakuja watu wengi, tunahitaji waje wengi pia siku hiyo ili kutupa hamasa wao ni wachezaji wa 12," alisema Skudu.

Hata hivyo, kiungo mkabaji wa timu hiyo, Zawadi Mauya, amesema mechi hiyo itakuwa ngumu kwani anaamini Azam haitokubali kuwa inafungwa mara kwa mara na Yanga.

"Utakuwa mchezo mgumu kwa sababu huwa tunawafunga sana Azam, hata mara ya mwisho kwenye fainali ya FA, sasa watakuja kivingine ili wasipoteze tena, ila siku zote kuipima timu yenu ipo vipi unahitaji mechi kama hizi na kingine nasema haitokuwa mechi rahisi kwa sababu nao wamefanya usajili mzuri kwa maingizo mapya ya wachezaji wao, lakini na sisi pia tuna usajili mpya na umekidhi matakwa, mazoezi yapo vizuri kuelekea kwenye mechi hiyo, nadhani baada ya hapo tutarudi ili kujiandaa na Ligi Kuu Agosti 15 na michuano ya kimataifa," alisema Mauya.

# *Simba Day haijawahi kutokea*

INATOKA UKURASA 24

mwandamizi zaidi kwenye kikosi cha Simba hivi sasa akiwa amedumu kwa misimu tisa tangu aliposajiliwa mwaka 2014 akitokea Kagera Sugar, hiyo ikiwa ni Simba Day yake ya 10.

### REKODI KUINGIA UWANJANI

Tamasha la Simba Day mwaka huu limeweka rekodi ya kujaza uwanja zikiwa zimebaki siku tatu kabla ya mchezo, na juzi mageti ya uwanjani hapo yalifunguliwa kuanzia saa 2:00 asubuhi ili kupunguza msongamano wa watu kuingia na kufikia saa 4:30 asubuhi tayari upande wa viti vya mzunguko vilikuwa vimeanza kujaa.

Hadi saa 6:00 mchana jukwaa la viti vya Orange mashabiki waliingia na kujaza nafasi hiyo, kufika saa 7:30 mchana uwanja ulikuwa umejaa.

### MCHEZO WA KIRAFIKI TIMU YA WANAWAKE NA VIJANA

Timu ya Simba Queens ilicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Masala Princess ambapo Malkia wa Wekundu wa Msimbazi hao waliibuka na ushindi wa mabao 4-0, yakifungwa na Asha Djafari aliyetupia mawili huku Joelle Bukuru na Shelda Boniface kila mmoja akifunga moja.

Kwa upande wa mechi ya vijana walicheza wenyewe kwa wenyewe huku timu ya kwanza ikipewa jina la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan na nyingine ikipewa jina la Makamu wa Rais Dk. Phillip Mpango.

Timu ya Rais Samia ikiwa imevalia jezi za rangi nyeupe ikinolewa na Selemani Matola na ya Makamu Rais, Dk. Mpango ilivaa uzi wa rangi nyekundu. Kikosi kilichopewa Samia Boys kiliibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Mpango Boys.

### BURUDANI KUANZA

Saa 5:35 asubuhi Burudani ya Muziki ilianza baada ya wasanii mbalimbali kupanda katika jukwaa maalum kwa ajili ya kuburudisha mashabiki 60,000 waliopo uwanjani.

Saa 6:17 mchana Bendi ya Twanga Pepeta inayomilikiwa na Mjumbe wa Bodi ya Simba, Asha Baraka ilitoa burudani kwa kuimba nyimbo ya 'Angurumapo Simba' ambayo ilikuwa kivutio cha mashabiki uwanjani hapo. Wasanii mbalimbali walitoa burudani akiwamo John Simon 'Joh Makini' na Meja Kunta, huku Tunda Man akitia fora kwenye tamasha hilo kwa kuingia kwa staili ya mfungwa na kibao chao cha 'Simba Sihami'.

Kikundi cha Sarakasi cha jijini Mwanza kilipanda Jukwaani saa 9:18 na kutoa burudani.

Ally Saleh 'Ali Kiba', ni msanii wa mwisho katika orodha ya watu waliotoa burudani ambapo alipanda jukwaa saa 9:37 na kukata kiu ya mashabiki waliojitokeza kwa wingi kushuhudia kikosi kipya cha 'Wekundu wa Msimbazi' hao wa msimu huu unaotarajiwa kuanza Agosti 9, mwaka huu.

### MENEJA WA IDARA YA HABARI NA MAWASILIANO AFUNIKA

Saa 10 :00 alasiri Ahmed Ally alifunika baada ya kuingia uwanjani na Ngamia kwa ajili ya kutambulisha wachezaji na benchi la ufundi.

Wachezaji Simba wanena:

Kiungo wa timu hiyo, Clatous Chama, alisema msimu huu wamejipanga kivingine kwa kila mchezaji kuhitaji kurejesha heshima ya klabu hiyo kwa kutwaa mataji ya ndani.

Alisema kwa muda ambao wako kambini kwa wale waliokuwapo msimu uliopita na wachezaji wapya wamekuwa na muunganiko mzuri na anaimani kufikia malengo yao kwa msimu wa 2023/24.

"Tunatakiwa kupambana kurudisha ubingwa wetu msimu huu, pia tuna kazi kubwa iliyopo mbele yetu kuvuka katika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kucheza nusu au fainali.

Beki wa timu hiyo, Che Fondoh Malone, alisema rangi pendwa kwake ni nyekundu na nyeupe ambayo anaamini Simba kwake ni sehemu sahihi na anaimani atafanya kile ambacho viongozi walishawishi kumsajili.

"Sitawaangusha benchi na viongozi kwa kunisajili, kikubwa tunahitaji kuwapa furaha mashabiki wetu wa Simba, kutwaa mataji na kufanya vizuri, ninaimani nimekuja kuimarisha 'Ukuta wa Yeriko' ndani ya timu yangu mpya," alisema Che Malone.

# Gamondi ataka mabao ya Simba

INATOKA UKURASA 24

cha ya kuendelea kutengeneza muunganiko wa kikosi chake pamoja na kuwataka wachezaji kutumia kila nafasi watakazozipata kufunga mabao.

Kikosi cha Yanga kinatarajia kuondoka leo kuelekea Tanga kwa ajili ya mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Azam FC, utakaopigwa keshokutwa, Jumatano kwenye Uwanja wa Mkwakwani.

ol

tar.
wa
simu
aada
ezaji
wa
kwa
lioni

Pep
ataji
lkay
hrez
pado
che-
oka,
Kyle
na
ajwa
ine.


## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 07/08/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4439 | QNK Quang Nam vs PHU Dong FC | 1.46 | 3.79 | 6.27 |
| 13:00 | 5817 | Dong Tam Long AN vs Binh Thuan | 1.54 | 3.78 | 5.05 |
| 13:30 | 2725 | Ansan Greeners vs Cheongju FC | 2.78 | 3.08 | 2.35 |
| 13:30 | 3820 | Australia W vs Denmark W | 1.89 | 3.31 | 3.71 |
| 14:00 | 5615 | Hirnik-Sport vs Yarud Mariupol | 2.46 | 3.12 | 2.62 |
| 15:00 | 3946 | Bali Utd Pusam vs Persik Kediri | 1.64 | 3.85 | 4.15 |
| 17:00 | 3238 | Bray Wanderers vs Longford Town | 1.53 | 3.89 | 5.05 |
| 17:00 | 3468 | Rosenborg BK 2 vs Kristiansund BK 2 | 1.64 | 4.43 | 3.63 |
| 17:00 | 5884 | Gjovik-Lyn vs Brann 2 | 1.74 | 4.23 | 3.33 |
| 18:00 | 2878 | FK Kauno Zalgiris B vs FK Ekranas | 3.64 | 3.74 | 1.76 |
| 18:00 | 3117 | FC KTP vs Inter Turku | 2.97 | 3.23 | 2.16 |
| 18:00 | 3444 | Vmfd Zalgiris-3 vs FK Vilnus Bfa | 2.24 | 3.44 | 2.68 |
| 18:00 | 4207 | Rabotnicki Sk vs Shkupi Skopje | 5.00 | 3.27 | 1.68 |
| 18:00 | 5547 | Lahti vs Honka | 3.88 | 3.32 | 1.81 |
| 18:00 | 5835 | Bayern Munchen vs Monaco | 1.37 | 4.60 | 5.80 |
| 18:30 | 1629 | Oppsal IF vs Tromso IL 2 | 2.05 | 3.83 | 2.77 |
| 18:30 | 3995 | Sepsi Osk vs FC Otelul Galati | 1.58 | 3.71 | 5.36 |
| 19:00 | 1158 | Breidablik Kopavogur W vs Thor Ka Akureyri W | 1.30 | 5.91 | 6.11 |
| 19:00 | 1362 | Viimsi JK vs JK Tabasalu | 1.58 | 4.72 | 4.41 |
| 19:00 | 2351 | Sandefjord Fotball 2 vs Fredrikstad FK 2 | 2.10 | 3.95 | 2.63 |
| 19:00 | 2556 | Arka Gdynia vs KP Polonia Warsaw | 1.71 | 3.54 | 4.14 |
| 19:00 | 2592 | Valur vs KA Akureyri | 1.61 | 4.04 | 4.29 |
| 19:00 | 3199 | Urartu vs Ararat Armenia | 2.68 | 3.04 | 2.51 |
| 19:00 | 4392 | Radnik Surduluca vs Spartak Subotica | 2.06 | 3.13 | 3.28 |
| 19:00 | 4718 | FK Panevezys vs FC Hegelmann Litauen Kaunas | 1.78 | 3.33 | 4.04 |
| 19:00 | 4859 | Galway United vs Treaty United | 1.10 | 6.86 | 18.16 |
| 19:00 | 4982 | Molde FK 2 vs Hodd 2 | 1.26 | 5.85 | 6.86 |
| 20:00 | 1667 | Malmo vs Halmstads BK | 1.25 | 5.06 | 9.11 |
| 20:00 | 2972 | Puszcza Niepolomice vs Stal Mielec | 2.29 | 3.13 | 2.83 |
| 20:00 | 3867 | Wexford Youths vs Waterford Utd | 7.25 | 4.94 | 1.30 |
| 20:00 | 4627 | Norrkoping vs IFK Goteborg | 2.11 | 3.23 | 3.07 |
| 20:00 | 5127 | Odense vs Viborg FF | 2.30 | 3.57 | 2.77 |
| 20:00 | 5180 | Trelleborgs FF vs Orebro SK | 2.34 | 3.25 | 2.99 |
| 20:00 | 5659 | Varbergs Bois vs Mjallby | 2.73 | 3.03 | 2.42 |
| 20:30 | 1282 | 07 Vestur Sorvagur vs B36 Torshavn | 3.74 | 3.53 | 1.79 |
| 21:00 | 1859 | Liverpool vs SV Darmstadt | 1.32 | 5.31 | 6.54 |
| 21:00 | 3354 | HFX Wanderers FC vs Pacific FC | 2.70 | 3.00 | 2.41 |
| 21:00 | 3453 | Kecskemeti TE vs Kisvarda FC | 2.32 | 3.36 | 2.70 |
| 21:00 | 3514 | Academia Cantolao vs Sport Huancayo | 3.84 | 3.28 | 1.84 |
| 21:00 | 3519 | Resovia Rzeszow vs Podbeskidzie Bie | 2.72 | 3.23 | 2.31 |
| 21:30 | 1375 | Voluntari vs Rapid Bucuresti | 3.07 | 3.17 | 2.23 |
| 21:30 | 2183 | Agropecuario vs Temperley | 1.97 | 2.99 | 3.87 |
| 21:30 | 4137 | CA Lugano vs Defensores Cambaceres | 2.80 | 2.75 | 2.49 |
| 21:30 | 5299 | Flandria vs Estudiantes Rio Cuarto | 2.90 | 2.80 | 2.51 |
| 21:45 | 1895 | Kerry FC vs Cobh Ramblers | 6.83 | 4.42 | 1.36 |
| 21:45 | 1958 | Larne vs Dungannon Swifts | 1.09 | 7.27 | 18.17 |
| 21:45 | 3764 | Athlone Town vs Finn Harps | 1.57 | 3.79 | 4.74 |
| 21:45 | 4071 | PAU FC vs Bordeaux | 3.72 | 3.32 | 1.92 |
| 23:00 | 2516 | FC Aguablanca vs Bogota FC | 2.46 | 2.91 | 2.86 |
| 23:15 | 1061 | Deportivo Garcilaso vs Deportivo Municipal | 1.27 | 4.85 | 8.48 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Agosti 7, 2023

Nipashe




Pochettino ataka Chelsea kwa Liver UKURASA 22

2023/24...



Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akipozi katika picha ya pamoja na kikosi kizima cha wachezaji wa Simba cha msimu wa 2023/24, wakati wa Tamasha la Simba Day, lililofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. Rais Samia alikuwa mgeni rasmi katika tamasha hilo lililohitimishwa kwa Simba kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Power Dynamos ya Zambia na kushinda mabao 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba Day babkubwa

## ●●● Rais Samia aituma mataji CAF, akiahidi tena mamilioni, Onana, Ngoma waiongoza kuirarua Dynamos...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba jana ilihitimisha kilele cha 15 cha Tamasha la Simba Day katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Power Dynamos ya Zambia.

**Hii inakuwa ni mara ya pili kwa Simba kuifunga timu hiyo kwenye kilele cha Simba Day, kwani mwaka 2019 iliichapa mabao 3-1 kwenye uwanja huo.**

Kwa ushindi huo, rekodi inayonesha kuwa katika michezo 15 ya tamasha hilo, imeshinda mara tisa, sare mara mbili na kufungwa mara nne.

Walikuwa ni wachezaji wapya kabisa waliosajiliwa msimu huu, Willy Essomba Onana na Fabrice Ngoma waliopeleka furaha Msimbazi kwenye tamasha hilo.

Mapema tu dakika ya nne Onana, raia wa Cameroon aliyesajiliwa kutoka Rayon Sport ya Rwanda alipachika bao baada ya kupokea pasi ndefu kutoka kwa Mzamiru Yassin akakimbia nao kwenye wingi ya kushoto, akaingia ndani kidogo kabla ya kuachia shuti la mguu wa kulia ukajaa wavuni.

Dakika ya 74, Ngoma aliyesajiliwa kutoka Al Hilal ya Sudan, aliipatia Simba bao la pili dakika ya 74, akiunganisha kwa kichwa krosi ya pembeni kutoka kwa Saido Ntibanzonkiza, ambaye alipigiwa kona fupi na Luis Miquissone.

Katika tamasha hilo ambalo mgeni rasmi alikuwa Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akihutubia mashabiki 60,000, waliofurika uwanjani hapo jana, ameaziahidi tena klabu zitakazoshiri michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba na Yanga na Kombe la Shirikisho, Azam FC na Singida Fountain Gate kuwa ahadi yake ya kutoa kiasi cha Sh. milioni tano kwa kila bao moja kama alivyofanya msimu uliopita ipo pale pale.

"Ahadi ipo pale pale, nendeni mkalete ushindi muiletee sifa Tanzania, ahadi ipo pale pale," alisema Rais Samia.

Alizipongeza Simba na Yanga kwa kufanya vema msimu uliopita kwa michuano ya kimataifa huku kuenda kufanya vizuri tena pamoja na Azam FC na Singida Fountain Gate.

**UTAMBULISHO WA WACHEZAJI**

Ulianza saa 10: 36 huku kubwa ikiwa ni zawadi ambayo haikutarajiwa na mashabiki utambulisho wa kipa mpya mzawa kutoka KMC FC, Hussein Abel, ambaye anaungana na makipa wengine wa klabu hiyo akiwamo Ahmed Feruz, Ally Salim na Aishi Manula.

Mabeki Shomari Kapombe, David Kameta, Jimmyson Mwanuke, Mohamed Hussein, Israel Patrick, Kennedy Juma, Hussein Kazi, Che Fondoh Malone na Henock Inonga Bacca.

Viungo ni Abdallah Hamis, Mzamiru Yasin, Sadio Kanoute, Nassoro Kapama, Fabrice Ngoma, Clatous Chama, Willy Essomba Onana, Aubin Kramo, Peter Banda, Saido Ntibazonkiza, na Kibu Denis huku washambuliaji wakiwa ni Shaban Chilunda, John Bocco, Mohamed Musa, Jean Baleke, Moses Phiri na Luis Miquissone.

Jumla ya wachezaji 30 wametambulishwa ambao wataitumikia Simba kwa msimu mpya wa 2023/24 na benchi la ufundi likiendelea kuwa chini ya Robertinho Oliveira.

Hili ni tamasha la 15 kufanywa na Simba tangu lilipoasisiwa na aliyekuwa Mwenyekiti wao, Mzee Hassan Dalali, pamoja na Katibu Mkuu mkuu wake, Mwina Kaduguda. Nahodha Msaidizi, Mohamed Hussein 'Tshabalala', ndiye mchezaji

INAENDELEA UKURASA 23

# Gamondi ataka mabao ya Simba

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amewataka washambuliaji wa timu hiyo kuhakikisha wanatengeneza rekodi kubwa ya kufunga mabao ya kutosha katika kila nafasi watakayoipata tofauti na msimu uliopita ambapo walizidiwa kwa ufungaji na wapinzani wao, Simba.

Ikumbukwe msimu uliopita Ligi Kuu Bara, Simba chini ya Robertinho Oliveira, ilihitimisha ligi hiyo ikiwa imefunga jumla ya mabao 75 ikimaliza katika nafasi ya pili wakati wapinzani wao, Yanga licha ya kuwa mabingwa walifunga jumla ya mabao 61 tu, jambo ambalo limemfanya Gamondi kuwatolea macho washambuliaji wa timu hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema moja ya mkakati wake mkubwa ni kuhakikisha washambuliaji wa timu hiyo wanaweza kufunga mabao mengi zaidi ili kuvunja rekodi ya wapinzani wao, Simba ya msimu ulioisha katika Ligi Kuu Bara licha ya wao kufanikiwa kuchukua ubingwa.

Alisema jambo muhimu ni kupata bao katika kila mchezo wa ligi ambao watacheza kwa sababu itawasaidia kupunguza presha kubwa kutoka kwa wapinzani.

"Jukumu la kwanza la kufunga lipo kwa washambuliaji halafu na kwa timu nzima katika kila nafasi ambayo itakuwa imepatikana kufanya hivyo, kuna kila sababu hasa upande wa safu ya ushambuliaji kuongeza kasi na umakini wa kutosha katika kutimiza majukumu yake.

"Nataka kuona wakifunga mabao mengi zaidi, angalia msimu ulioisha licha ya kushinda ubingwa, timu ilizidiwa mabao mengi na wapinzani jambo ambalo sihitaji kuona likijirudia kwa sasa, msimu ujao unaelekea utakuwa wa ushindani kwa kila timu kujipanga vizuri," alisema Gamondi.

Aliongeza kuwa maelekezo hayo kila mchezaji anayajua li-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >